**ATCL** yapokea ndege ya 14, Majaliwa aonya ukatishaji ruti



UKURASA 2

**Serikali** yazuia kiwanda cha chai cha Mo kufungwa

UKURASA 5

**Mke** adaiwa kupata tatizo la akili mume kudhulumu nyumba yake

UKURASA 7



UKURASA 22

**VINICIUS: NAHISI KUKOSA HAMU YA KUCHEZA**

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatano Machi 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581628

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



CAG mstaafu, Ludovick Utouh

## CAG MSTAAFU ALONGA:

# Kuna ulegevu kuwajibisha wanaotajwa

**Na Ludovick Utouh**

KWA kipindi cha miaka minane nilichofanya kazi kama CAG (2006 hadi 2014), nilishuhudia ugumu uliopo wa kuwachukulia hatua watumishi wa umma waliofuja fedha za umma ama kusababishia hasara serikali.

Wasiwasi wangu huu umethibitishwa na kauli ya Rais Samia kwenye kauli yake aliyoitoa wakati akipokea ripoti za CAG Machi 2023 aliposema....

ENDELEA UKURASA 4



Sehemu ya Bonde la Msimbazi, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Simulizi walioambulia 'kiduchu' bomoabomoa Bonde Msimbazi

• **Aliyetarajia** mil. 200/- aambulia mil. 16/; mwenzake asafisha uso kwa 27,000/-... *Endelea ukurasa wa 8*

## P DIDDY ATOWEKA, USALAMA WAVAMIA NYUMBA ZAKE

**LOS ANGELES,** Marekani

MAWAKALA wa Usalama wa Marekani jana walivamia jumba la rapa, Sean "Diddy" Combs au Puff Daddy lililoko...



UKURASA 24

## Taasisi dini zatajwa utakatishaji fedha na ufadhili wa ugaidi

UKURASA 2

**MICHEZO** **PIGO AL AHLY, MAMELODI, KICHEKO SIMBA, YANGA** UK.24

**KATUNI** UK.6



Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi (aliyesimama) akifungua mafunzo kwa wanawake vijana kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na maamuzi katika ofisi za Mtandao huo, Jijini Dar es Salaam juzi, ambapo palikuwapo washiriki 97 kutoka vyuo 11 nchini. **PICHA:TGNP**

# Taasisi za dini nchini zatajwa utakatishaji

**Na Beatrice Shayo**

TANZANIA imetajwa haina mifumo mizuri ya usimamizi na ufuatiliaji mienendo wa jumuiya za kiraia, zikiwamo taasisi na madhehebu ya dini, hali inayotengeneza hatari ya kutumika katika utakatishaji fedha haramu au kufadhili ugaidi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamadi Masauni, wakati akizindua kampeni za usajili wa jumuiya nchini.

Alisema baadhi ya jumuiya za kiraia zimeripotiwa kujihusisha au kutumika katika kufanikisha kutendeka kwa makosa ya jinai na vitendo vingine vyenye madhara kwa jamii.

Alitaja miongoni mwa makosa hayo ni utakatishaji fedha haramu, ugaidi na ufadhili wa shughuli za kigaidi, usafirishaji haramu wa binadamu, biashara haramu ya silaha na kuwapo jumuiya za kidini zinazotoa mafundisho potofu na hatarishi kwa usalama wa raia (afya ya mwili na akili).

"Madhara yatokanayo na kuchelewa kutoa ufumbuzi wa changamoto nilizozitaja hapo juu pamoja na udhaifu wa mifumo ya fedha katika taasisi hizo, umepelekea Taasisi ya Kimataifa ya Financial Action Task Force (FATF) ambayo ilianzishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kutoa ripoti ambayo inaonesha kuwa nchi yetu haina mifumo mizuri ya usimamizi na ufuatiliaji mienendo wa jumuiya za kiraia, zikiwamo taasisi na madhehebu ya dini.

"Hali hiyo inatengeneza mazingira rafiki ya taasisi hizo kutumika au kuwa katika hatari ya kutumika katika utakatishaji fedha haramu au kufadhili masuala ya ugaidi," alisema.

Waziri huyo aliitaja ni hali iliyosababisha Tanzania kuwekwa katika kundi la nchi zinazohitaji ufuatiliaji wa karibu (Enhanced Monitoring).

"Hivyo, ni lazima tushirikiane kwa karibu katika kuondoa hali hii kwenye nchi yetu," alisema Masauni na kuongeza kuwa vyombo vya kimataifa na wadau mbalimbali wa kimataifa wamekuwa wanapewa tahadhari kuhusu udhaifu wa kusimamia jumuiya hizo ambao unaweza kutumika katika masuala utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Waziri Masauni alisema hali hiyo inaweza kuleta madhara ya kuharibu taswira nzuri ya kidiplomasia iliyomo katika nchi.

"Ninaendelea kusisitiza umuhimu wenu katika kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya inatekeleza Mpango Kazi wa FATF utakaowezesha serikali kuondolewa kwenye kundi hili, pia kufanikisha jukumu la kudumisha amani na utulivu katika maeneo yetu," alisema.

Waziri Masauni alisema licha ya faida alizozitaja zitokanazo na jumuiya zilizosajiliwa, hivi karibuni kumeibuka wimbi la kutumia jumuiya za kiraia katika kufanya vitendo vinavyohatarisha amani na usalama wa nchi.

Waziri alisema kuna baadhi ya jumuiya zinatumika katika kusaidia makundi yenye dhima ya kigaidi, kusambaza propaganda za uchochezi, kuwasilisha ajenda za kigeni au wafadhili wa nje ambao ajenda zao zinaweza kuhatarisha maslahi ya taifa ikiwamo mmonyoko wa maadili.

Alisema ni muhimu kwa jumuiya za kiraia kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni za maadili, uwazi na uwajibikaji ili kuhakikisha wanachangia katika maendeleo ya jamii bila kuhatarisha ulinzi na usalama wa nchi au kusababisha mmonyoko wa maadili.

Alieleza kuwa serikali ina jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli za jumuiya za kiraia ili kuhakikisha zinafanya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi.

Waziri huyo pia alisema kumebainika changamoto ya uanzishwaji holela na utitiri wa nyumba za ibada katika maeneo mbalimbali nchini.

"Baadhi ya jumuiya za dini, hususan makanisa na misikiti, zimebainika kujengwa katikati ya makazi ya watu, kuna mrundikano wa taasisi nyingi kwenye eneo dogo na baadhi ya taasisi kutumia sauti za juu na hivyo kusababisha adha na usumbufu katika jamii," alisema.

Kwa upande mwwingine, waziri huyo alisema jumuiya za kiraia zina mchango mkubwa katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kuchangia katika maendeleo endelevu ya jamii na taifa kwa ujumla katika kuchochea ubunifu na ukuaji wa uchumi, utoaji huduma za kijamii, zikiwamo za elimu na afya.

Alisema jumuiya za kiraia zilizosajiliwa zina uwezo wa kushirikiana na serikali, mashirika ya kimataifa na wadau wengine katika kutekeleza miradi na shughuli za maendeleo.

Alieleza kuwa usajili unaweza kuwa muhimu katika kuanzisha ushirikiano na kupata rasilimali na msaada kutoka kwa wadau hao na kudumuisha uwazi na uwajibikaji.

"Ni lazima kisheria kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha za mapato na matumizi ya jumuiya ambazo hutakiwa kuwasilishwa na kupitishwa na wanachama kupitia mikutano mikuu ya jumuiya zao kabla ya kuwasilishwa katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya,"aliagiza.

Alsiema wizara yake imekuwa inashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufanya kazi kwa karibu na ofisi za makatibu tawala wa mikoa na ofisi za wakuu wa wilaya katika ufuatiliaji mienendo na usimamizi wa jumuiya kupitia kamati za usalama zilizoko katika ngazi za mikoa na wilaya.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sospeter Mtwale, alisema watashirikiana na wizara na kuchukua hatua dhidi ya jumuiya ambazo zinakwenda kinyume cha taratibu za nchi.

# ATCL yapokea ndege ya 14, PM aonya ukatishaji ruti

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Ndege ya Tanzania (ATCL), imepokea ndege ya 14 huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa maagizo saba likiwamo la kupunguza ukatishaji wa ruti za ndani.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana Dar es Salaam wakati wa mapokezi ya ndege mpya ya kisasa aina ya Boeing 737-9 MAX.

Waziri Mkuu aliwaagiza viongozi na watendaji wa shirika hilo kupunguza kukatisha ruti za safari za ndege nchini ili kuleta matumaini makubwa kwa watumiaji wa ndege hizo.

Pia aliwaagiza kuhakikisha ndege zinaendeshwa kwa tija kwa kufanya utafiti wa kutosha wa masoko kabla ya kuzipeleka.

Maagizo mengine ni wahakikishe mikoa yote inaunganishwa na safari za ndege na kuendelea kutafuta fursa za safari za kimataifa ili kuongeza fedha za kigeni.

Kwa upande wa Wizara ya Uchukuzi, Majaliwa alitaka kusimamia ipasavyo kampuni hiyo ili kuhakikisha uwekezaji mkubwa uliofanywa unaendelea kuleta matokeo chanya.

"Watumishi wetu ongezeni uzalendo na kila mmoja athamini kazi inayofanywa na serikali. Muwafichue wale wote wenye nia ovu ya kuhujumu uwekezaji huu pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato kupitia tiketi na mizigo katika maeneo yetu ya kufanyia mauzo," aliagiza.

Kadhalika aliitaka wizara kuandaa mpango wa kuongeza watalaam wazalendo ambapo mbali ya kupeleka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), waje na ubunifu kupitia vyuo vingine vya ndani kwa fani zinazohusika.

Maagizo mengine aliyatoa kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) akitaka waongeze udhibiti wa usalama wa ndege kwa kuhakikisha wahudumu na wahandisi wanakuwa na sifa za kuhudumu ndege za kimataifa.

"Saba, taasisi na wadau wote katika viwanja vya ndege wahakikishe wanashiriki kikamilifu na kuwa sehemu ya kuimarisha huduma hii," aliagiza na kusema serikali itaendelea kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iendelee kusimamia bodi za taasisi za serikali kufikia malengo.

"Hivi karibuni tutaanza safari ya ndege ya Dubai na Afrika Kusini. Katika kipindi cha miaka mitatu hatuwezi kuacha kuwaambia mafanikio ujenzi wa reli ya kisasa hivi sasa umefikia kilomita 2102," alisema.

Alisema wakati serikali ikinunua ndege, wanaimarisha ujenzi wa viwanja vya ndege, kikiwamo cha Msalato kitakachounganisha safari za ndani na mataifa ya nje ya nchi na gharama za ujenzi Sh. bilioni 360 ambao umefikia asilimia 54.01 na unatarajia kukamilika Novemba 2025.

Pia alisema wanakiimarisha Kiwanja cha Julius Nyerere Dar es Salaam ili kukifanya kuwa kitovu cha usafiri wa anga Afrika Mashariki kwa kuongeza miruko katika mataifa mbalimbali.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema serikali imenunua ndege mbili za mafunzo kwa ajili ya NIT ili kutoa mafunzo kwa marubani na kupunguza uhaba wao.

Pia alisema chuo hicho kimewezeshwa mitambo ya kisasa ili kuzalisha wahandisi na mafundi mchundo kuondoa uhaba wa wataalam katika sekta ndogo ya usafiri.

Mtendaji Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema kampuni hiyo inaendelea kutekeleza mpango mkakati wake wa pili wa miaka mitano ulioanza 2022/23 na utamalizika mwaka wa fedha 2026/27.

Alisema mpango huo unahusisha mpango wa tatu wa taifa wa miaka mitano 2021/22 -2025/26 na wanatarajia kuwa na ndege 20 ikiwamo hiyo iliyopokelewa ambapo hadi sasa ATCL ina ndege 14 zilizonunuliwa katika kipindi cha ufufuaji ikiwamo ndogo iliyokuwako kabla ya ufufuaji na kufanya kuwa na ndege 15.

Alisema ndege ya 16 ambayo ni ya masafa marefu inatarajiwa kupokelewa mwezi Aprili, mwaka huu, na ya jana ni kwa ajili ya safari za masafa ya kati.

Alisema uwapo wa ATCL umechochea matumizi ya usafiri wa anga na kufanya kutoonekana ni kitu cha anasa na mahitaji ya miruko ndani ya nchi ni makubwa na bado kuna uhitaji katika baadhi ya vituo vinavyotarajiwa kufunguliwa.

"Ajira zimeongezeka kutoka 175 wakiwamo marubani ni 13, wahandisi 27 na watumishi wengine 131 kwa mwaka 2016 hadi ajira 780 wakiwamo marubani 117, wahandisi 151 na watumishi wengine 512 kufikia mwezi Februari 2024," alisema.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wake, Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema Rais Samia anapotimiza miaka mitatu ya uongozi, wana kila sababu ya kutembea kifua mbele.

"Kwa niaba ya chama na nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa RC Dar es Salaam (Albert) Chalamila hapa, amenifurahisha. Kuna kasumba ya ujinga unaoendelea ya kutaka kumtofautisha Dk. Samia (Suluhu Hassan) na Dk. (John) Magufuli huwezi kuwatenganisha hawa watu.

"Na viongozi wengi wanafiki wanaotaka kujipendekeza kwa Rais Samia kila wakipata jukwaa wanataka kumfanya (Samia) kama si sehemu ya Dk. Magufuli.

"Kama msemaji wa chama, tuna ilani, kila anachofanya Dk. Samia ndicho alichofanya Dk. Magufuli, walizunguka nchini nzima kutafuta kura, huwezi kuwatenganisha na Waziri Mkuu wao yule pale, Kassim Majaliwa.

"Ningetamani leo iwe mwisho wa unafiki wa viongozi na wanasiasa uchwara wanaopambana kuwatenganisha viongozi hawa, mafanikio haya tunasherekea wote," alisema Makonda.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salam, Albert Chalamila, alisema ni heshima kwa Rais Samia kuendelea kuyafanya mambo ambayo waliyokwisha kuyafanya (Samia na Magufuli).

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Habari njema
Jambo letu kubwa linakaribia...
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

MAKALA MAALUM

# Kuna ulegevu wa kisheria kuwajibisha watumishi wanaotajwa ripoti za CAG

**Na Ludovick Utouh**

WATANZANIA waipendao nchi yao na wanaoitakia maendeleo chanya, wanasubiri kwa shauku kubwa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23 zitakazowasilishwa bungeni mwezi Aprili 2024 na kuwa wazi kwa umma.

Katika ripoti za mwaka 2021/22 zilizowasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan Machi 29, 2023, mbali na kuwa kulikuwa na uboreshwaji mkubwa wa hati za ukaguzi zilizotolewa na CAG, bado kuliripotiwa vitendo vingi vya matumizi mabaya na upotevu wa fedha za umma.

Akiongea baada ya kupokea ripoti hizo, Rais Samia alionesha kukasirishwa na hali hiyo na kuagiza wahusika wa vitendo hivyo wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

"Nadhani tumezubaa kwenye "punitive measures", hatuchukui hatua kwenye adhabu, ingekuwa tunachukua hatua haya yasingeendelea. CAG wewe majalada unampelekea Kamishna wa Mashtaka (DPP), ninaomba kasi ya adhabu za kisheria iongezeke," alisema Rais Dk. Samia siku hiyo.

Mwishoni mwa mwezi Machi 2024, itakuwa ni mwaka mmoja umeisha tangu ripoti za CAG za mwaka 2021/22 zipokewe na Rais na kuwasilishwa bungeni. Sasa ni muda wa kupokea ripoti mpya za CAG za mwaka 2022/23.

Shauku iliyopo kwa Watanzania ni je, hali ya mwaka huu itakuwa tofauti na miaka mingine? Je, maagizo ya Rais yametekelezwa? Je, hali ya uadilifu na uzalendo miongoni mwa watumishi wa umma imeongezeka, hivyo kusababisha kupungua kwa vitendo vya ubadhirifu, uwizi na ufujaji fedha za umma?

WAJIBU (taasisi anayoiongoza) inaipongeza serikali kwa kuongeza uwazi zaidi kwenye hatua zinazochukuliwa katika kutekeleza mapendekezo yanayotolewa na CAG.

Kwa uelewa wa WAJIBU, taarifa za CAG ni tathmini ya kina ya utendaji wa mifumo ya usimamizi ya ndani, utekelezaji sera na mipango pamoja na namna serikali ilivyokusanya na kutumia fedha za umma kwa kipindi kinachoripotiwa.

Hivyo, ni muhimu kwa maofisa masuuli na watumishi wengine wa serikali kuzichambua kwa kina ripoti za CAG kwa lengo la kuendelea kuboresha utendaji wa serikali kwa vipindi vijavyo.

WAJIBU imekuwa inafanya uchambuzi wa ripoti zinazotolewa na CAG kwa kipindi za miaka saba mfululizo (2015/16 hadi 2021/22). Katika uchambuzi wa ripoti hizo, WAJIBU imebaini mambo makuu saba yafuatayo:

Kwanza; kumekuwa na mwenendo hafifu wa utekelezaji mapendekezo ya CAG. Katika kipindi cha miaka saba cha uchambuzi wa ripoti hizo, utekelezaji wa mapendekezo yake umekuwa chini ya asilimia 50.

Mara nyingi, ama bungeni au serikalini kumekuwa na kauli au migongano ya kimtazamo baina ya viongozi wa juu wanaohusika katika usimamizi wa utekelezaji mapendekezo ya CAG.



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2021/22, kutoka kwake CAG Charles Kichere, Ikulu jijini Dar es Salaam Machi 2023. **PICHA: MAKTABA**

Mara kadhaa, ama bungeni au serikalini yamesikika maneno ya kushuku juu ya usahihi wa mapendekezo au hoja zinazoibuliwa na CAG.

Hali hii tunaamini inasababishwa na kutokuwa na uelewa au kuwapo ukakasi katika utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika kuzishughulikia hoja za ukaguzi zinatokana na ripoti za CAG.

Kwa mujibu wa Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009 (The Public Audit Regulations 2009), Kifungu cha 93 kinamtaka kila ofisa masuuli (accounting officer) kuandaa majibu ya hoja za CAG ndani ya siku 21 baada ya ripoti ya CAG kuwasilishwa bungeni na kuwa wazi kwa umma. Hivyo, kwa mujibu wa kanuni hiyo, maofisa masuuli ndio wenye mamlaka ya kutoa majibu juu ya hoja za ukaguzi na siyo mawaziri au wanasiasa.

Ushauri wangu juu ya hili ni kuwa, "TUSIWE MABINGWA WA KUPINGA HOJA ZA UKAGUZI BALI TUJITAHIDI KUWA MABINGWA WA KUZUIA HOJA ZA UKAGUZI KUJITOKEZA". Tukiliweza hilo, shughuli zote za serikali zitakuwa zinafanywa kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo ambapo hoja za ukaguzi zitapungua kwa kiasi kikubwa.

Pili; kumekuwapo uboreshaji mkubwa wa uandishi/utayarishaji hesabu za serikali katika ngazi zote za serikali kwa kuzingatia hati za ukaguzi zinazotolewa na CAG.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inastahili pongezi za kipekee kwa kuona umuhimu wa uandaaji taarifa za fedha na hesabu za serikali kuzingatia viwango vya uhasibu vya kimataifa kuanzia mwaka 2004, uamuzi ambao umechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha hali ya uandishi wa hesabu za serikali nchini.

WAJIBU katika uchambuzi wake wa ripoti za CAG, na kupitia ripoti zake za "Hali ya Uwajibikaji wa Kifedha Nchini" (CASFAR) za mwaka 2019/20 na 2020/21, inaonesha maboresho makubwa ya hati za ukaguzi zilizotolewa na CAG.

Kwa mfano, matokeo ya ukaguzi wa CAG kwa kipindi cha miaka mitatu (2019/20 - 2021/22) yanaonesha maboresho katika uandaaji hesabu kwa Serikali Kuu, mashirika ya umma pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii imepelekea kuongezeka kwa idadi ya taasisi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na mashirika ya umma yaliyopata hati safi.

Kwa mwaka 2019/20, hati safi kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mashirika ya umma na serikali kuu zilikuwa asilimia 87, mwaka 2020/21 zilikuwa asilimia 95 na mwaka 2021/22 asilimia 96.

Tatu; upungufu makubwa katika utendaji wa mfumo mzima wa ukaguzi wa ndani. Katika ripoti zote za CAG zimeonesha utendaji hafifu wa vitengo na mfumo mzima wa ukaguzi wa ndani kutokana na sababu mbalimbali kama kukosekana kwa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi, kutokuwa na ujuzi stahiki, utendaji duni wa kamati za ukaguzi na mfumo duni wa kutoa taarifa (reporting mechanism).

Upungufu wa utendaji wa mfumo mzima wa ukaguzi wa ndani pia unaweza kuonekana kwa kuwapo hoja zinazotokana na uzingatiaji duni wa sheria, taratibu na kanuni za utendaji katika utumishi wa umma.

Nne; ulegevu wa sheria na kanuni za usimamizi wa rasilimali katika kuwachukulia hatua watumishi waliohusika kwenye kuvunja sheria, taratibu na kanuni za utendaji katika utumishi wa umma.

Kwa kipindi cha miaka minane nilichofanya kazi kama CAG (2006 hadi 2014), nilishuhudia ugumu uliopo wa kuwachukulia hatua watumishi wa umma waliofuja fedha za umma ama kuisababishia hasara serikali.

Wasiwasi wangu huu umethibitishwa na kauli ya Rais Samia kwenye kauli yake aliyoitoa wakati akipokea ripoti za CAG Machi 2023 aliposema, "Nadhani tumezubaa kwenye 'punitive measures', hatuchukui hatua kwenye adhabu, ingekuwa tunachukua hatua haya yasingeendelea."

Hii inatokana na ukweli kwamba sheria zetu hazitoi taratibu bayana za kuchukuliwa hatua kwa watumishi wa aina hiyo na wakati mwingine taratibu zilizowekwa za kushughulikiwa mambo haya kiutawala huwa ni mrefu mno na si rahisi kutekelezeka "not effective".

Mfano, itakumbukwa kwenye miaka ya nyuma, Kamati ya Bunge ya Usimamizi wa Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), chini ya uenyekiti wa Agustino Mrema ilikuwa inaagiza maofisa masuuli na watumishi wa umma waliotajwa kuhusika na upotevu wa fedha za umma katika ripoti za CAG wakatwe asilimia fulani ya mishahara yao, ingawaje agizo hilo lilikuwa ni kinyume cha sheria na kanuni za utumishi wa umma.

Hali hii ilitokana na kukosekana hatua stahiki zinazotosheleza kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa upotevu wa fedha na rasilimali nyingine za umma. Hali hii inaonekana ilikuwa ni tatizo hata kwenye nchi nyingine kama vile Marekani, Uingereza, Afrika ya Kusini na hata majirani zetu Kenya.

Kwenye miaka ya 2006 na kuendelea walilazimika kutunga sheria za kupambana na vitendo vya matumizi mabaya ya fedha za umma (Fraud Acts) katika jitihada za kuimarisha utaratibu wa kisheria wa kushughulikia vitendo vya uwizi, ufisadi na ubadhirifu wa fedha za umma.

Tano; kumekuwa na wimbi kubwa la vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma. Baada ya kuchambua ripoti za CAG, Taasisi ya WAJIBU imekuwa inafanya tathmini ya miamala ambayo ina viashiria vya vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu. Ingawa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, miamala hiyo imekuwa inapungua, bado jumla yake ni kiasi kikubwa cha fedha.

Mathalani kwa mwaka 2021/22, ripoti za CAG zilizotolewa mwezi Machi 2023, zinaonesha jumla ya miamala ya Sh. trilioni 3.05 (Sh. trilioni 4.59 mwaka 2020/21) ina viashiria vya rushwa, udanyanyifu na ubadhirifu ambayo ni sawa na asilimia tisa (9) na 13 ya matumizi yote ya serikali, mtawalia.

Vitendo hivi vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu vinaendelea kuwapo kutokana na udhaifu wa utendaji kazi wa taasisi za uchunguzi na mashtaka kushindwa kuchunguza kwa wakati matukio ya rushwa, kupata ushahidi stahiki na kushtaki kwa wakati watuhumiwa wote wa vitendo hivi.

Vilevile, kumekuwapo na tatizo kubwa la kupungua kwa uzalendo, uadilifu na kumekuwapo na tabia ya kutotii sheria, kanuni na miongozo inayotolewa kwa ajili ya kuendesha shughuli za serikali.

Sita; katika ripoti zote za CAG za miaka saba iliyopita, imeripotiwa kuwa mashirika ya umma na taasisi za serikali zimekuwa na matatizo makubwa ya utegemezi kwa serikali, kushindwa kujiendesha, kutofikia malengo ya kuanzishwa kwake pamoja na kujiendesha kwa hasara.

Katika uchambuzi wake, WAJIBU imebaini sababu mbalimbali zinazopelekea changamoto hizo, kubwa zikiwa ni; udhaifu katika uongozi wa taasisi na mashirika hayo, kuwapo mikataba na taratibu za kiutendaji zinazozuia ufanisi kati ya serikali na taasisi au mashirika hayo, uhaba wa mitaji na kuingiliwa kiuendeshaji na kiutendaji wa mashirika na taasisi hizi za umma na mamlaka mbalimbali za serikali na vyama vya siasa.

Saba; kumekuwa na uboreshwaji mkubwa wa usimamizi wa rasilimali za umma hasa kutokana na utekelezwaji wa Mpango Mkakati wa Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP - programs) pamoja na uimarishaji mifumo ya kielektroniki (MUSE) uliofanyika hasa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

*Mwandishi wa makala hii ni CAG mstaafu, pia alishakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na Mhadhiri wa Uhasibu Chuo Kikuu cha Mzumbe.

**FUATILIA KESHO USHAURI WAKE KWA SERIKALI**

# Serikali yakataa kufungwa kiwanda cha Mo Enterprises

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imekataa kuridhia ombi la kufungwa kwa kiwanda cha chai cha Mo Enterprises na viwanda vingine nchini kuepusha athari kwenye sekta ya ajira na uwekezaji nchini.

Pia, imesema ili sekta ya chai isonge mbele, iko tayari kuwapokonya mashamba ya chai wawekezaji walioshindwa kuyaendeleza ili kunusuru sekta hiyo.

Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, akizungumza kwenye mkutano wa bodi ya chai jijini hapa, alisema kuna athari nyingi za kufunga viwanda kwa watu mbalimbali ambao wamewekeza, ikiwamo baadhi ya watu kukosa ajira.

Bashe alisema atakaa chini na viongozi wa kiwanda hicho kuona kero zinazowakabili ili waweze kuzitatua na shughuli za uzalishaji ziendelee.

"Hatutakubali kufunga viwanda badala yake tutakaa chini na kujadiliana kuona tunafanya nini," alisema Bashe.

Alisema kuna kero nyingi ambazo serikali wanakutana nazo, lakini wanaendelea kuzifanyia kazi ili ziweze kuondolewa.

Pia, walipokea ombi la kufungwa viwanda kutoka kwa MO Enterprises, lakini hawajakubaliana nalo na badala yake watakaa chini kuzungumza na wadau.

Alisema wizara yake inaendelea na vikao na Wizara ya Fedha ili kuona wanachohitaji kwa ajili ya sekta ya chai waweze kusaidiwa.

"Tunaendelea na vikao na Wizara ya Fedha tutafikia mwafaka ili tuweze kuingia sekta ya chai hapa nchini," alisema Bashe.

Alisema hakuna kitu kinachoshindikana mbele ya serikali watajipanga kupiga hatua moja mbele kwenye sekta hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Chai, Mary Kipeja alisema, wakulima wadogo wa zao hilo wanaidai serikali Sh. bilioni 2.8 kwenye viwanda jambo linalowarudisha nyuma.

Alisema fedha hizo ni nyingi na wameiomba serikali kusimamia ili waweze kupata fedha zao.

"Wakulima wadogo wanadai fedha zao kutoka kwa viwanda, naomba suala hilo lifanyiwe kazi ili wakulima wapate haki yao," alisema Kipeja.

Kadhalika, alisema wakulima wanaweka jitihada kubwa katika kilimo hicho, lakini wanakatisha tamaa kutokana na kutokupata fedha zao kwa wakati.

# Ngome ya Wanawake ACT yakomaa na NEC

**Na Mwandishi Wetu**

NGOME ya Wanawake ya Chama cha ACT Wazalendo imesema sehemu ya waathirika wakubwa wa udanganyifu katika uchaguzi nchini ni wanawake, ikipanga kuzunguka nchi nzima kushawishi wanawake na makundi mbalimbali kuhakikisha nchi inapata Tume Huru ya Uchaguzi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa ngome hiyo, Janeth Rithe, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuunga mkono kauli iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa chama chao ya kutaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ijiuzulu kutokana na madai ya kufanya kazi kwa upendeleo.

Rithe alisema viongozi wanaopatikana kwa ridhaa ya wanachi wana jukumu la kuhakikisha wanawatumikia wananchi na kutatua kero zao huku wakitambua mwajiri wao namba moja ni mwananchi (Ibara ya 8 ya Katiba ya nchi).

"Tunapokuwa na viongozi wanaoingia madarakani kwa udhaifu wa tume ya uchaguzi ni wazi hawatawatumikia wananchi na matokeo yake ujinga, maradhi na umaskini utatamalaki miongoni mwetu na waathirika wakubwa tunakuwa sisi wanawake.

"Ngome ya Wanawake tunakubaliana na kauli ya chama kuwa kwa vile muundo na utaratibu mpya wa kupatikana kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa njia ya ushindani ulipitishwa na Bunge kupitia Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, tume iliyopo ijiuzulu kupisha tume mpya ya uchaguzi kuteuliwa," alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa uchaguzi wa hivi karibuni wa marudio katika kata 23 uliofanyika tarehe 20 Machi mwaka huu, umewaonyesha bayana kuwa tume ya sasa haiwezi kusimamia Uchaguzi Mkuu kwa ufanisi kwa sababu upatikanaji, muundo na mwenendo wake unakibeba chama tawala badala ya kusimamia maslahi ya wananchi.

"Kwenye uchaguzi huo wa marudio Ngome ya Wanawake tulipangiwa na chama kusimamia kampeni za uchaguzi katika Kata ya Kabwe iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

"Tumeshuhudia pia wasimamizi wa uchaguzi, wengi wakiwa makada wa Chama Cha Mapinduzi wakisaidia CCM ishinde ikiwamo kwa kubadili namba kwenye vituo ambavyo ACT Wazalendo tulishinda," alisema.

Aliongeza kuwa kinachowasikitisha ni kuona viongozi wa juu wa nchi wakikaa kimya pale wananchi wanaponyimwa haki yao ya msingi ya kuchagua kiongozi wanayemtaka.


## Lindi Jumbo Limited
TANZANIA

Lindi Jumbo
Limited

**EOI RREFERENCE NUMBER - LJL_2024-19**
**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR BULK SUPPLY AND DELIVERY of FLOCCULANTS AND FROTHERS**

The Lindi Jumbo Graphite project is situated in southeastern Tanzania, about 200 km away from the port of Mtwara. The project area can be accessed from the southern part via sealed roads that lead from Mtwara to Nanganga, which is approximately 15 km to the north of the town of Ruangwa.

**DESCRIPTION OF THE SCOPE OF THE PRODUCTS:**
Lindi Jumbo Limited is seeking expressions of interest from companies capable of supplying and delivering the following.

| Reference # | Item Description |
|---|---|
| LJL_2024-19 | **The frother:** |
| | Polyethylene Glycol Monobutyl Ether (Butyl-TriGlycol) Mixture, molecular weight approximately 200 g/mol. Dow 200, Flotanol 200, Sasfroth 200, Senfroth 200 or equivalent. Supplied in 1000 IBC. Consumption 1000 kg/month. |
| | |
| | **The flocculant:** |
| | Poly acrylamide flocculent, Senfloc 5150, Flopam AN912SH or equivalent. Supplied in 25 kg bags, 40 bags on a pallet. Consumption 1000 kg/month |

**Objectives:**
The primary objectives of The Contractor are as follows:

1. **Timely Delivery:** Ensure the punctual supply and delivery of Flocculants and Frothers to Lindi Jumbo's specified location(s) as per the agreed-upon schedule to minimise downtime and disruptions to operations.
2. **Quality Assurance:** Provide products that meet or exceed the required quality standards and specifications outlined by Lindi Jumbo, ensuring consistency and effectiveness in their application within the mining processes.
3. **Reliability and Consistency:** Maintain consistent supply capabilities to fulfil Lindi Jumbo's ongoing operational needs, avoiding stockouts or delays in product availability that could impact production schedules.
4. **Communication and Transparency:** Maintain open and transparent communication channels with Lindi Jumbo's procurement and operational teams, providing regular updates on order status, product availability, and any potential issues or concerns.
5. **Compliance:** Adhere to all relevant regulatory and compliance requirements, including but not limited to environmental, health, safety, and legal regulations governing the supply and handling of chemical products in Tanzania.
6. **Cost-effectiveness:** Offer competitive pricing structures and cost-effective solutions while maintaining the quality and reliability of the supplied products and services, optimising overall operational expenditures for Lindi Jumbo.
7. **Technical Support:** Provide technical support and assistance as needed, including product training, troubleshooting, and on-site support to ensure the effective utilisation of Flocculants and Frothers within Lindi Jumbo's mining processes.
8. **Sustainability:** Demonstrate a commitment to sustainable practices throughout the supply chain, including environmentally responsible sourcing, packaging, and disposal of products, aligning with Lindi Jumbo's sustainability objectives.
9. **Customer Service:** Maintain a high level of customer service and responsiveness, addressing any inquiries, concerns, or issues promptly and effectively to ensure a positive and productive business relationship with Lindi Jumbo.
10. **Continuous Improvement:** Strive for continuous improvement in supply chain efficiency, product quality, and service delivery through feedback mechanisms, performance evaluations, and collaborative problem-solving with Lindi Jumbo's procurement and operational teams.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**

1. Proof of registration with the Tanzania Revenue Authority (TRA).
2. Company Information - including but not limited to corporate details, trading name, company registration number, official report from BRELA, Local Content Compliance, and Tax Clearance Certificate for the latest year.
3. Company profile.
4. Capability Statement.
5. Copy of certificates of accreditation with other operations.
6. List of Insurances, where applicable.
7. Quality Assurance Plan.
8. Material Safety Data Sheets
9. Previously historical supply the same products.
10. Dealership letter from the OEM or JV with local Tanzanian indigenous company

Companies that possess the ability, capacity, and resources to supply the specified products are invited to express their interest by uploading their proposals via the Procurement portal, **www.webportunities.net.**
Please note that only proposals submitted via the portal will be evaluated.

All documents must be submitted in English on or before 4:00PM (GMT +1) on 12 April 2024. Should you require assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team via the portal's Contact Us page.

Lindi Jumbo Limited will review and assess the documents provided by interested companies in accordance with this Expression of Interest (EOI). Evaluations will be conducted based on internal criteria to determine which companies will be included in the list of pre-qualified companies. Only the pre-qualified companies will receive an invitation to bid by signing a Non-Disclosure Agreement (NDA) as part of the call for tender process continuation.

Please be informed that Lindi Jumbo Limited is not bound to accept the lowest or any tender offer received, and the adjudication of the tender will be based solely on the discretion of the company with consideration given to both qualification and commercial aspects.

We look forward to receiving your expression of interest and potentially partnering with your company for the supply and delivery of these essential products.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Itungwe sheria kali kuwadhibiti wabadhirifu wa fedha za umma

**TAARIFA** kuhusu ubadhirifu, wizi na uchepushaji wa fedha katika mamlaka za serikali za mitaa nchini, zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara huku zikionyesha kwamba baadhi ya wahusika wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Kwa ujumla kuendelea kuwapo watu hao na vitendo kama hivyo kujirudia kila uchao, kunakwamisha nia njema ya serikali kupeleka fedha katika halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha hizo ambazo zimekuwa zikiripotiwa kuibwa baadhi ni zile za mapato ya ndani katika halmashauri na zingine kutoka serikali kuu zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama afya, elimu, barabara na maji.

Kila viongozi wa juu kama Rais, makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanapofanya ziara katika maeneo mbalimbali kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo, mambo hayo yamekuwa yakiripotiwa na wahusika kuchukuliwa hatua. Pamoja na hatua zinazochukuliwa, inaonekana kuwa tatizo hilo ni sawa na ugonjwa sugu kwa kuwa watu wamekuwa wakiendelea kutumbua tu fedha za umma.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipofanya ziara mkoani Kigoma, aligundua wizi wa kutisha wa fedha za miradi huku baadhi ya miradi iliyopewa fedha hizi imetekelezwa chini ya kiwango. Bila kusita, Waziri Mkuu aliagiza wahusika wote wachukuliwe hatua ikiwamo kuchunguzwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kama vile haitoshi, alipofanya ziara mkoani Mara, mambo kama hayo yalijirudia na mbaya zaidi ikabainika kuwa baadhi ya watendaji hao ngazi ya halmashauri, wana mtandao wa ushirikiano na maofisa katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Hiyo ilibainika baada ya ofisa mmoja aliyechukua fedha na kukutana na maofisa wa TAMISEMI katika mji mmoja kisha kugawana.

Jambo hilo la kuwapo kwa mtandao baina ya baadhi ya watendaji wa halmashauri na maofisa wa TAMISEMI limebainika baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kutoa kauli hiyo ikiwa katika ziara Muheza mkoani Tanga. Kamati hiyo imebainisha wazi kwamba baadhi ya maofisa katika ofisi hiyo ya Rais wanawalinda wabadhirifu wa fedha kwenye halmashauri kwa kuwakumbatia ili wasichukuliwe hatua.

Mwenyekiti wa LAAC, Halima Mdee, alisema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akifanya majumuisho ya ziara kwa kuzungumza na watumishi wa halmashauri baada ya kukagua ujenzi wa shule ya sekondari na hospitali ya wilaya. Alisema hali hiyo ya kulindana inatokana na uswahiba baina ya watumishi wa TAMISEMI na halmashauri na huo ni mtandao wa kuiba fedha za umma zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.


Kwa ujumla, hadithi ya kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha katika halmashauri si mpya kwa kuwa imekuwa ikielezwa kila mwaka na hata ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka husika, zimekuwa zikijirudia.

Hatua hiyo inaonyesha kwamba tatizo hilo ni sugu na halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Hali hiyo imekuwa ikisababisha miradi mingi ya serikali kufanyika katika kiwango duni na mingine kutokukamilika na matokeo yake wananchi kuendelea kupata adha ya ukosefu wa huduma mbalimbali.

Wahenga wanasema penye nia pana njia. Kwa mantiki hiyo kama kweli kuna nia ya dhati ya kukomesha vitendo kama hivyo, hapana budi kuchukuliwa hatua dhidi ya wahusika kwa kuwa vitendo kama hivyo ni uhujumu wa Uchumi. Kwa mantiki hiyo, serikali ifanye mabadiliko ya sheria kwa kuwaingiza watu hao kwenye kundi la uhujumu uchumi.

Ni imani kwamba kama hiyo itafanyika na wahusika wa wizi na ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi za serikali wakafikishwa mahakamani na kuhukumiwa, ni wazi kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa. Watu wanaopewa dhamana ya kusimamia fedha hizo watakuwa na nidhamu wakiamini kwamba wakifanya makosa, sheria itawahusu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Hivi ndivyo Magufuli, aliiacha nchi katika mikono salama ya Samia

**LEO** ni siku ya 10 tangu kufanyika kwa kumbukumbu ya miaka mitatu ya kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, hayati Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17 mwaka 2021.

Pamoja na kwamba ni siku ya 10 tangu kufanyika kumbukumbu ya kifo chake, huku mengi yakiwa yameandikwa kuhusu utendaji wake, ninadhani si vibaya kuendelea kumkumbuka zaidi.

Kwa leo ninataka angalau nikumbushe kidogo jinsi ambavyo aliiweka Tanzania yenye uchumi wa kipato cha kati, ambao unaendelezwa na mrithi wake Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni mwaka 2020 ndio ambao Benki ya Dunia iliiorodhesha Tanzania kuwa katika orodha ya nchi za uchumi wa kipato cha kati kutokana na vigezo mbalimbali vilivyowekwa na benki hiyo.

Tanzania ilitangazwa kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati mapema kabla ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambao serikali ilijiwekea kuwa ingetimia mwaka 2025, lakini hilo likatimia mapema.

Hatua hiyo ilionyesha ni jinsi gani nchi inapiga hatua kwenda mbele katika maendeleo. Hivyo, wakati huu ambao Watanzania wanajiandaa na kumbukumbu ya kifo chake, ni vyema pia kuangalia jitihada za kiongozi huyo za kulisaidia taifa kupiga hatua mbalimbali za kimaendeleo.

Mbali na kukabiliana na ufujaji wa fedha, Dk. Magufuli alifanikiwa kudhibiti matumizi ya fedha na ufujaji wa fedha hizo kufanikiwa kufikia malengo mapema kabla ya mwaka 2025.

Lakini pia, lengo la kuifanya nchi kuwa ya viwanda, ni miongoni mwa jitihada zilizoifanya Tanzania kuwa ya kipato cha kati, kwani serikali iliandaa mpango wa miaka mitano wa maendeleo ya taifa.

Mpango huo pamoja na mengine, ulisisitiza ujenzi wa viwanda ambavyo vitachangia ukuaji wa uchumi na kutatua changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana wengi wasio na ajira nchini.

Wadau mbalimbali wa maendeleo, waliitikia azma hiyo ya serikali na hivyo miradi mbalimbali ya maendeleo ikaanzishwa vikiwamo viwanda na vingine vya zamani vikawa vinafufuliwa.

Kitendo cha kutangazwa Tanzania kuwa ya uchumi wa kipato cha kati, kilimfanya Rais kutoa wito kwa Watanzania kuendelea kuchapa kazi zaidi ili kuzidi kujiweka katika mazingira mazuri.

Tanzania ikatajwa kuwa miongoni mwa nchi 50 duniani na nchi ya 24 kwa Afrika na ya pili kwa Afrika Mashariki kuwa ya uchumi wa kipato hicho, huku akiwa na kaulimbiu ya 'Hapa Kazi tu'. Lakini Rais Samia naye ameendeleza kaulimbiu hiyo kwa namna nyingine ya 'Kazi Iendelee'.

Ni wazi kwamba uchumi wa kipato cha kati ni ishara ya umaskini umepungua, uchumi imara unajengwa, uzalishaji viwandani unaimarika na wananchi wanapata maendeleo.

Vilevile, uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati inayokuza uchumi, kuwekeza kwenye maendeleo ya watu na kujenga sekta binafsi yenye tija kwa maendeleo ya taifa, vimeifikisha Tanzania ilipo sasa.

'Hapa Kazi tu na Kazi Iendelee' ni kaulimbiu ambazo zinahimiza ufanyakazi kwa bidii, iwe ofisini, viwandani na kwingineko, kila mmoja anatakiwa kufanya kazi kujiletea maendeleo na kukuza uchumi wa taifa.

Watanzania wanapokumbuka miaka mitatu ya kifo cha Magufuli, wanakumbuka pia jinsi alivyohimiza uchapakazi na kujitahidi kuibua miradi mbalimbali ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Juhudi hizo ndizo zilizowezesha nchi kutangazwa ya uchumi wa kipato cha kati, Rais Samia anapita katika nyayo hizo kwa kukaribisha wawekezaji kwenye sekta mbalimbali ili kukuza uchumi wa nchi.

# Mke adaiwa kupata tatizo la akili mume kudhulumu nyumba yake

**Na Neema Hussein,**
KATAVI

MKAZI wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Felsta Mathias, anadaiwa kupatwa na tatizo la afya ya akili baada ya kutapeliwa mali na mume wake alizozitafuta kipindi walipotengana.

Ayubu Isaya (23), mtoto wa pili kati ya sita katika familia ya mama huyo, alisema walihamia Mpanda baada ya mama yao kutengana na baba yao kutokana na kipigo alichokuwa akikipata kutoka kwa baba yao wakati wanaishi Halmashauri ya Mpimbwe.

Alisema mama yake aliamua kukimbilia Mpanda na kumuacha mume wake na kuanza kujishughulisha na biashara ndogo za kuuza, nyanya, vitunguu na vitu vingine vilivyomuwezesha kupata pesa na kununua kiwanja na kuanza kujenga boma.

Hata hivyo, mama yake alipogoma kurudiana na mume wake, baba yake alifungua kesi mahakamani na kutokana na kukosekana maelewano mahakama iliamuru wapeane talaka kisha wagawane mali ikiwamo nyumba aliyojenga mwanamke huyo Mpanda ambayo ilikua haijamalizika.

“Mahakama ilimpa nyumba ya zamani mama na nyumba mpya aliyokuwa akijenga alipewa baba na watoto tukaamriwa kuishi kwa baba na kutimiziwa mahitaji yote ikiwamo kuendelea kusoma kitu ambacho baba hakukifanya,” alisema.

Isaya alisema, baada mama yake kuona kiwanja alichonunua na nyumba yake kupewa mume wake, alikata rufani, ndipo alipoanza kupata tatizo la akili na baba yao alipoona hivyo, alitumia fursa hiyo kuuza kiwanja na boma alilopewa na mahakama.

Isaya aliendelea kusimulia kuwa mama yake alikuwa akimfundisha biashara ya kuuza nyanya na vitunguu na baada ya kupatwa na tatizo hilo ameendelea kufanya biashara hiyo huku akilea wadogo zake.

Aidha, kupitia michango ya wadau, ilimwezesha kumpeleka mama yao hospitali Dodoma kwa uchunguzi zaidi na kurejea kwenye hali yake ya kawaida na kuanza biashara, lakini baada ya muda hali ile ilirudi kutokana na kukosa pesa za kumpeleka kliniki kila baada ya miezi mitatu.

Alisema kutokana na changamoto za ugumu wa maisha wanazopitia ombi lao kubwa kwa jamii na serikali ni msaada wa pesa kwaajili ya matibabu ya mama yao na wadogo zake kupata elimu pamoja na kuongezewa mtaji wa kuendeleza biashara alioachiwa na mama yake ili asaidie familia.

Scholastika Isaya (12), mwanafunzi wa darasa la sita, mtoto wa nne katika familia ya mama huyo, alisema wanaomba msaada mama yao apate matibabu kutokana na hali yake kuzidi kuwa mbaya kufikia hatua ya kuchoma magodoro.

“Makonda alipokuja nilienda, baada ya kuona kwenye taarifa ya habari kuna mtoto mmoja huko Kigoma kujieleza na kusaidiwa na mimi nilivyoona nikasema nikienda nitasaidiwa, lakini sikupata nafasi ya kuongea naye,” alisema.

“Siku iliyofuata nilirudi nikaonana na wasaidizi wake wakasema watamsaidia mama kumpeleka hospitali, tunaomba sana serikali itusaidie mama apelekwe hospitali na nyumba yake arudishiwe nasisi tukae kwenye hali nzuri sasahivi mama analala chini nyumba inavuja,” alilalamika mtoto huyo.

Dina Yotham, mfanyabiashara katika soko la Mpanda ambaye alikuwa akifanya biashara na mama huyo, alisema kilio chake kikubwa alichokua akimsimulia ni kuhusu kudhulumiwa nyumba na mume wake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tambukareli, Selestino Shalutanga, amesema tukio hilo analifahamu na familia hiyo ilifika kwake kuomba msaada, walichangishana lakini pesa haikutosha kufanikisha matibabu ya mama huyo.

# Mahakama Kuu yatengua hukumu ya Mahakama ya Kisutu malipo mil. 100/-

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, imetengua hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyomtaka mfanyabiashara Sudhir Lakhanpal kumlipa aliyekuwa Mkurugenzi mwenza, Azim Hooda, Sh. milioni 100 alizokopeshwa.

Jaji John Nkwabi alifikia uamuzi huo baada ya kukubali rufaa iliyowasilishwa na mrufani Lakhanpal, kupinga uamuzi wa Mahakama ya Kisutu ambayo ilikubali maombi ya mjibu rufaa Hooda.

Jaji Nkwabi alisema, ameridhika kuwa Mahakama ya Kisutu ilifanya makosa kumpa mjibu rufani Sh. milioni 100, na hukumu na amri ya mahakama hiyo inatupiliwa mbali.

Jaji huyo alibainisha kuwa hakuwa na uhakika ni lini hasa mrufani aliomba mkopo na hakukuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa mrufani aliomba mkopo huo kutoka kwa mjibu rufaa.

“Nimeridhika kuwa kesi ya mjibu rufani ilikuwa na mikanganyiko isiyoweza kusuluhishwa katika ushahidi wa kila shahidi wake na jumla ya ushahidi uliotolewa wakati wa kusikilizwa shauri hili na Mahakama ya Kisutu,” alisema Jaji Nkwabi.

Alisema kuwa shahidi mmoja alionesha kuwa fedha hizo zilikabidhiwa kwa mrufani ndani ya muda mfupi, lakini ushahidi mwingine unaeleza kuwa ilichukua zaidi ya miezi saba.

Pia, alibainisha kuwa mjibu rufani anadai kuwa ni rafiki wa mrufani, lakini inaonekana alikuwa na undugu na mjibu rufani kupitia Kampuni ya Regalia.

“Inahitaji ushahidi kwa mtu kukubali kwamba mtu anayefanya kazi katika taasisi moja ni rafiki wa mwingine, kwa sababu si kawaida kwamba kila mtu anayefanya kazi katika taasisi moja ni marafiki,” Jaji alisema.

Wakati wa kusikilizwa kwa rufani hiyo, wakili wa upande wa mrufani, Joseph Rutabingwa, alisema kuwa ikiwa kweli mjibu rufani alitoa mkopo kwa mrufani, kwanini alitoa maelezo yanayokinzana kuhusu tarehe na awamu mbele ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Kisutu.

Kwa upande mwingine, mjibu rufani alidai kuwa mrufani kupokea kiasi hicho cha mkopo wakati anafanya kazi katika kampuni yake inayoitwa Regalia Tanzania Limited kama mkurugenzi na hajawahi kulipa.

Ilidaiwa kuwa mjibu rufani alimshtaki mrufani kwa madai ya aina mbalimbali, ikiwa ni pamoja na malipo ya Sh. milioni 100 kama mkopo uliotolewa kwake kwa kuwa walikuwa wanafahamiana na marafiki wa karibu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

## MIKATABA YA UNUNUZI WA MAHINDI MEUPE (NON-GMO) NA MPUNGA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula Nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, NFRA hununua nafaka kwa ajili ya Akiba ya Taifa ya chakula.

NFRA inatarajia kununua Mahindi Meupe na Mpunga katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2024/2025, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024. Ununuzi huo utafanyika kwenye maghala yaliyopo kanda za Arusha (ghala la Arusha na Babati), Dodoma (ghala la Dodoma na Manyoni), Kipawa (Dar es Salaam), Makambako, Songwe, Shinyanga, Songea na Sumbawanga (Sumbawanga na Mpanda) na vituo vingine ambavyo vitafunguliwa na Wakala.

Aidha, ili kuongeza wigo wa kufikia ununuzi wa tani 700,000 pamoja na kuwa na utaratibu wenye tija katika shughuli za ununuzi msimu wa 2024/2025, NFRA itaingia Mikataba ya Ununuzi wa nafaka (Framework Agreement) na Wakulima pamoja na Wafanyabiashara wenye sifa zilizoainishwa hapa chini.

**1. MASHARTI KWA MKULIMA:**

i) Mkulima awe na shamba kuanzia ekari 100 ndani ya eneo moja katika Halmashauri/Wilaya na kuwepo na uthibitisho huo kutoka Serikali ya Kijiji/Halmashauri ya Wilaya ya shamba lilipo.

ii) Mkulima awe na uwezo wa kuzalisha kuanzia tani 200 za Mahindi Meupe au Mpunga.

**2. MASHARTI KWA MFANYABIASHARA:**

Mfanyabiashara lazima atimize masharti yafuatayo;
a. Awe na uwezo wa kuiuzia NFRA kuanzia tani 2,000 hadi 5,000 za Mahindi Meupe au Mpunga.
b. Hati hai ya kutodaiwa kodi (valid tax clearance)

**3. MASHARTI YA UJUMLA:**

i) Mwombaji anapaswa kuwasilisha uthibitisho wa; -
a. Uraia au kampuni iliyosajiliwa Tanzania;
b. Namba ya Mlipa Kodi (TIN) na kuwa tayari kulipa kodi za Serikali;
c. Leseni ya biashara ya mazao;
d. Barua ya utambulisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri wa eneo ambalo Muombaji anafanya shughuli zake za kilimo au biashara;
e. Utayari wa kuridhia kuuza nafaka yake kwa bei itakayopangwa na NFRA;
f. Utayari wa kuridhia kuwasilisha Mahindi au Mpunga katika ghala/kituo atakachoelekezwa na kwa muda atakaopangiwa kwa mujibu wa Mkataba atakaoingia na NFRA;
g. Mahali salama pakuhifadhia Mpunga au Mahindi Meupe kabla ya kununuliwa na NFRA;
h. Kuzingatia vigezo vya ubora wa Mpunga na Mahindi Meupe daraja la kwanza vilivyowekwa na NFRA kwa mujibu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

ii) Mwombaji anaelekezwa kuwasilisha barua ya maombi ya kuiuzia NFRA Mpunga au Mahindi Meupe kabla au ifikapo tarehe 20 Aprili, 2024. Barua husika iwasilishwe kwa Mameneja wa Kanda kwa njia ya barua pepe au anuani za ofisi za Kanda zilizokaribu na Mwombaji au anapokusudia kuwasilisha nafaka zake.

iii) Barua ya maombi iainishe yafuatayo; jina na anuani ya mwombaji, namba ya simu, baruapepe, kiasi cha Mpunga au Mahindi Meupe anayokusudia kuuzia NFRA na kituo anachopendekeza kuwasilisha Mpunga au Mahindi Meupe.

iv) Waombaji watakaofuzu vigezo na masharti wataingia mikataba na NFRA ya kuuza Mpunga au Mahindi Meupe kwa kuzingatia uhitaji wa nafaka kutoka kwa NFRA (framework contract), kuanzia tarehe 1 Mei 2024.

Tanbihi: Mkulima/Mfanyabiashara asiye na vigezo tajwa hapo ataendelea kuuza nafaka zake kwa kuwasilisha katika maghala makuu ya NFRA yaliyopo katika Ofisi za Kanda au vituo vya ununuzi vitakavyofunguliwa na NFRA, pasipo kuwa na mikataba hii ya ununuzi kutoka NFRA.

Kwa taarifa zaidi Mwombaji anaweza kuwasiliana na NFRA kupitia **simu namba +255 (0) 26 2963953** au Baruapepe: **info@nfra.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**
**Tarehe 25 Machi, 2024.**

# Simulizi walioambulia 'kiduchu' bomoabomoa Bonde la Msimbazi

## • Aliyetarajia fidia ya mil. 200/- aambulia mil. 16/-
## • Mwenzake asafisha uso wake kwa fidia ya 27,000/-

**Na Beatrice Shayo**

NYUMBA 2,155 zilizomo katika Bonde la Msimbazi, jijini Dar es Salaam zinatarajiwa kubomolewa kuanzia Aprili 12, mwaka huu baada ya wamiliki wake kulipwa fidia ya Sh. bilioni 52.61 kupisha mradi wa kuendeleza bonde hilo.

Hata hivyo, taarifa za bomoabomoa hiyo zimeibua kilio kwa baadhi ya wananchi, wakiwamo wapangaji wa nyumba zilizoko eneo hilo, wakidai wenye nyumba wamechukua kodi licha ya kuwa na taarifa kwamba nyumba zao zitabomolewa.

Mjumbe wa Shina Mtaa wa Madaba, Jamila Juma, akizungumza na Nipashe juzi, alisema ni miongoni mwa waliogomea fidia ya awali ambayo aliandikiwa kulipwa Sh. milioni saba, jambo ambalo hakuridhishwa nalo.

Alisema kwa sasa amelipwa fidia ya Sh. milioni 12 na baada ya muda aliongezwa Sh. milioni nne ambazo alijulishwa wameongezwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema fedha aliyolipwa imeishia kununua kiwanja na hakuwa anajua nyumba yake itabomolewa Aprili 12, mwaka huu, jambo ambalo limemshangaza.

Jamila alisema awali walijulishwa kuwa katika mradi huo, fidia ya nyumba ni Sh. milioni 200, lakini walicholipwa ni tofauti na uhalisia wa maisha.

"Nilikuwa na matumaini ya Sh. milioni 200, kama ningekosa hiyo, basi wangesema kila mmoja wanamlipa Sh. milioni 50 ambao tuna nyumba ili ununue kiwanja na kujenga, matokeo yake tumeambulia fedha kiduchu, yupo mtu aliyelipwa Sh. 27,000, huu mradi umekuja na maumivu," alisema.

Agustina Francis (54), alisema bado hajalipwa fidia kwa kuwa awali walimwambia fidia yake ni Sh. milioni saba, akawagomea na alivyofanyiwa tathmini nyingine, anasuburia kulipwa Sh. milioni 38.

Mpangaji katika eneo hilo, Veronica William, alisema hana taarifa ya kubomolewa nyumba, mwenye nyumba amekuwa anapokea kodi huku akiwajulisha nyumba hiyo haiwezi kubomolewa.

"Mimi nimesikia baba mwenye nyumba kalipwa fidia, lakini hajatuambia wapangaji wake tunatakiwa kuondoka, amekuwa hata mkataba hatupatii, kodi tumemlipa. Kwahiyo, zinakuja kubomolewa Aprili 12, hata hatujui.

"Jamani, ninakushukuru kwa kuniambia, maana ningedhalilika wangekuja kutubomolea na mali zetu zingepotea daah! Ngoja nianze kutafuta nyumba nyingine, jamani! Mbaya ni huyu baba mwenye nyumba, anachukua kodi na kukaa kimya," alilalama.

**BIL. 52/- ZA FIDIA**

Mratibu wa miradi ya ushirikiano na Benki ya Dunia (WB) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Humphrey Kanyenye, aliwaambia waandishi wa habari jijini juzi kuwa watu 2,155 kati ya 2,329 waliomo kwenye daftari la kwanza wamekwishapokea malipo yao ya Sh. bilioni 52.61 kupisha mradi wa kuendeleza bonde hilo.

"Hii 'yard' ya mabasi ya mwendokasi itahamishiwa Ubungo Maziwa, ni sehemu ya kazi ya mkandarasi, lengo la mradi huu ni kujenga mto kwa ajili ya kuzuia mafuriko yanayotokea katika eneo hilo na tutajenga City Park (Maegesho ya Jiji) ambayo itaongoza kwa ukubwa," alitamba.

Mratibu huyo alisema mradi huo una mambo matatu; kujenga daraja, ujenzi wa mto na kuhamisha kituo cha mabasi ya mwendokasi na kujenga Maegesho ya Jiji, ukigharimu Dola za Marekani milioni 260.

Kanyenye alisema ofisi ya uratibu wa mradi kwa kushirikiana na ofisi za wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni wanatarajia kuanza ubomoaji nyumba zilizofidiwa kuanzia Aprili 12, mwaka huu, yaani siku 17 zijazo.

Alisema awamu hiyo ya utekelezaji zoezi hilo itawahusu wale ambao wamefikishwa wiki sita zilizotolewa baada ya kupokea malipo ya fidia hadi kufikia Februari 29, mwaka huu.

Alisema daftari la pili la waathirika 446 ambao hawakufikiwa katika uthamini wa awali kwa sababu ya kugomea fidia hiyo na kudai ni ndogo kwa sasa wameshakubali na kutia saini.

Alisema daftari lilitarajiwa kuwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutiwa saini jana Machi 26, mwaka huu.

"Wananchi ambao wana maswali au wanahitaji maelezo zaidi kuhusu ubomoaji wanaweza kuwasiliana na ofisi ya uratibu wa mradi wa Bonde la Msimbazi kupitia namba ya WhatsApp 0738353854 kwa kutuma ujumbe au kupiga namba 0738353855 kupata majibu ya maswali yote kuhusiana na mradi huo," alisema.

**HABARI HII ILIPASWA KUTOKA TOLEO LETU LA JANA LAKINI KULITOKEA TATIZO LA KIUFUNDI. TUNAOMBA RADHI KWA USUMBUFU ULIOJITOKEZA. MHARIRI.**



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, (wa pili kushoto), akipokea msaada wa vifaa vya afya ya mama na mtoto kutoka kwa Mwalikilishi wa Mkurugenzi wa Jhpiego, Dk. Mteule Amon, jijini kwenye ofisi ya Mkuu huyo, jana. Kulia ni Mratibu wa mradi wa USAID Afya Yangu Kanda ya Dar es Salaam, Joyce Ishengoma na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ayoub Kibao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Polisi wamsaka dereva wa lori la ajali iliyoua waandishi wa habari

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

WAANDISHI wa Habari wawili wamefariki dunia na mwingine kujeruhiwa katika ajali ya gari iliyotokea eneo la Chumbi, Wilaya ya Rufiji, mkoani Pwani.

Waliofariki dunia katika ajali hiyo ni waandishi wa habari wa Mkoa wa Lindi ambao walikuwa safarini wakitokea jijini Dar es Salaam kurejea katika mkoa wao wa kikazi Lindi.

Ajali hiyo ambayo ilitokea usiku wa kuamkia jana, ilisababisha vifo vya Josephine Kibirity, Mwandishi wa Kampuni ya Sahara Media Group na Abdallah Nanda wa Chanel Ten.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Rufiji, SACP Protas Mutayoba alisema waandishi hao walikuwa wanasafiri kwa kutumia gari dogo ambalo liligongana na lori huko Chumbi.

Alisema miili ya marehemu hao imehifadhiwa Kituo cha Afya Ikwiriri. Majeruhi Mziray Abed anaendelea kupatiwa matibabu Hospitali ya Wilaya (Utete).

Kamanda Mutayoba alisema dereva wa lori lililogongana na gari hilo alitoroka baada ya ajali na anaendelea kutafutwa ili aeleze kilichotokea katika ajali hiyo.

Waandishi hao ni kati ya wawakilishi washiriki wa mafunzo yaliyokuwa yanatolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kutoka Mkoa wa Lindi.

# ...Wizara yaingilia kati wakazi 1,700 kuondolewa kwa nguvu KIA

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

ZIKIBAKI siku nne kufika ukomo wa notisi ya siku 21 kwa wakazi 1,712 wa vijiji vinane vya Wilaya ya Hai kuondolewa kwa nguvu ndani ya ardhi ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Wizara ya Uchukuzi imeingilia kati na kuagiza mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kupeleka mapendekezo yao.

Machi 10, mwaka huu, Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO), ilitoa notisi hiyo ya kutaka wananchi hao kuondoka kwa hiari kabla ya kuondolewa kwa nguvu na kutakiwa kulipa gharama zote zitakazoambatana na kazi hiyo.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema kwa kuwa jambo hilo lilikuwa limepangwa na mikoa hiyo miwili na KADCO, wizara hiyo imetoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa husika kukaa tena na kuja na mapendekezo yao, ambayo wizara itayafanyia kazi ili kuangalia maslahi ya wananchi na KADCO.

"Mbunge wa jimbo hilo, aliomba nyongeza ya siku 90. Tumefanya mawasiliano serikali za mikoa na wizara. Tumewataka wakae tena na mapendekezo yao tutayafanyia kazi.

"Bado wananchi 85 hawajalipwa, kati ya hao wapo wananchi 28, ambao hawajalipwa kwa sababu ya vitambulisho. Wananchi watano mashauri yao yako mahakamani, yanasubiri mirathi na 17 wameweka kusudio la kuweka zuio la mahakama na wamegoma kuchukua fedha na 31 hawakuweza kupatikana," alisema. Wakati Naibu Waziri Kihenzile akithibitisha hayo, KADCO kupitia notisi hiyo, imeeleza ulipaji kifuta jasho ili kuondoka ndani ya eneo la KIA, uliwahusisha wananchi wa vijiji vya Sanya Station, Tindigani, Chemka, Mtakuja, Majengo Kati, Kaloleni, Samaria na Malula.

Notisi hiyo iliyoanza kuhesabiwa kuanzia Machi 11, mwaka huu, inafikia ukomo wake Machi 31, mwaka huu. Aprili Mosi, mwaka huu, wananchi watakaokuwa wamekaidi maelekezo hayo, wataondolewa na kulipa gharama zote zitakazoambatana.

Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe, aliwasilisha ombi maalum la nyongeza ya muda kwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyekuwa mkoani Kilimanjaro wiki iliyopita.



## Kituo cha Afya Sale chapokea msaada vifaa vya upasuaji

**Na Allan Isack,**
NGORONGORO

WANANCHI wa Kata ya Sale iliyoko Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, wataanza kunufaika na huduma za matibabu, baada ya serikali kupeleka vifaa tiba vya upasuaji katika Kituo cha Afya Sale.

Lengo la serikali kupeleka vifaa tiba hivyo ni kusogeza huduma ya upasuaji kwa wananchi wa Kata za Malambo, Pinyinyi, Oldonyosambu na Sale.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo, alisema serikali imejitahidi kupeleka miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo, ikiwamo kuboresha miundombinu ya kijamii hasa sekta ya afya kwa kutoa vifaa tiba ambavyo vitasaidia kuokoa maisha ya watu.

"Serikali imeleta shilingi milioni 370 kwa ajili ya kununua vifaa hivi na kuelekeza kuletwa katika kituo hiki cha afya ili kifanye ya kuhakikisha kinatoa huduma kwa wananchi," alisema Kanali Sakulo.

Vilevile alitoa rai kwa uongozi wa kata na kijjiji kwa kuboresha na kudumisha ulinzi katika eneo la kituo hicho cha afya ili vifaa hivyo vidumu.

"Nataka ulinzi uimarishwe hapa, kwa kuwa tunatakiwa kuvilinda vifaa hivi kwa kuwa vinathamani kubwa na vina tija kwetu sote," aliongeza Kanali Sakulo.

Diwani wa Kata ya Sale, Hamza Masedo, alisema serikali ya imejitoa katika kuboresha miradi ya maendeleo na katika mpango wa kujali afya za Watanzania.

# Ushiriki mdogo wa wasichana mafunzo ya uanagenzi waikwamisha serikali

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema ushiriki mdogo wa wasichana katika programu ya mafunzo ya uanagenzi nchini, unatishia mustakabali wa mpango wa serikali wa kupata wataalam wa kutosha wa mitambo na zana za kilimo.

Programu ya uanagenzi iliyoanzishwa na serikali mwaka 2016 kwa Sheria ya Bunge ya Mwaka 2012 na baadae Tangazo la Serikali Namba 153 la Mei 4 Mwaka 2012, inayolenga kuwezesha utoaji wa ujuzi na stadi muhimu zinazohitajika katika viwanda.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara katika kikao kati ya wafadhili wa mradi huo, Shirika la West Germany Chambers of Craft & Skilled Traders Council (WHKT) na wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA),

Mwakilishi wa wizara hiyo, Ezekiel Kunyaranyara, alisema kikwazo kikubwa wanachokiona katika utekelezaji wa mradi huo kwa sasa ni ushiriki mdogo wa vijana wa kike.

"Imebidi tuje na mpango mahususi wa tatizo hili na tumeshaweka mkakati kwamba mpaka kufikia mwaka 2026, wataanza kuvipima vyuo vya VETA kwa kuingiza idadi kubwa ya watoto wa kike.

"Mtazamo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ni kuongeza usaili wa wasichana kwa asilimia 50, ambacho kitakuwa kipimo." alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa VETA, Abdalla Ngodu, katika programu hiyo wasichana 43 pekee kati ya vijana 362 waliodahiliwa kujiunga na vyuo vitano vya ufundi nchini, ndio waliopenya katika mpango huo wa mafunzo ya fani ya mitambo na zana za kilimo.

Ngodu, alitoa mfano wa VETA-Manyara, ambacho kwenye mradi huo kilidahili vijana 133, lakini wasichana waliopata fursa hawakuzidi sita.

Alivitaja vyuo vilivyonufaika na programu hiyo ni Manyara, Arusha, Dakawa, Mpanda na Kilakala.

"Tumepata vifaa vya udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya kuvunwa ambavyo vitawanufaisha wakulima, lakini pia tumepata vifaa vya karakana, ambavyo vitasaidia kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa; ambavyo vilikuwa vinatumiwa na walimu walionolewa na Wajerumani," alifafanua.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo la Taifa, Vrajil Jituson, alisema vijana wanaopata ujuzi wanakuwa bora kuliko hata waliomaliza vyuo vikuu.

Alisema shida kubwa inayowakabili ni hawana vifaa vya kufanyia kazi na wengi wao wanahitaji mitaji ili wajikwamue kiuchumi.

Aidha, Meneja mradi kutoka Ujerumani, Herman Roeder alisema alipoanzisha mradi huo alipata ushirikiano mkubwa.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi (katikati), akikata utepe kufungua zahanati mpya ya Matela, katika kijiji cha Singa, wilayani Moshi juzi. Kushoto ni Mkuu wa wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Serikali yatumia mil.410/- kurejesha ufaulu shule 16

**Na Steven William,**
MUHEZA

JINAMIZI lililokuwa likiziteſa shule 16 za sekondari za Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, kutofanya vizuri katika mitihani ya taifa kutokana na kukosa vifaa vya maabara na vitabu vya sayansi, limeilazimisha serikali kutumia zaidi ya Sh. milioni 410 kupata mwarobaini wake.

Mkuu wa wilaya hiyo, Zaina Abdallah, alisema uamuzi wa serikali kumaliza tatizo hilo, unalenga kuinua ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa sekondari, hasa wasichana.

Zaina aliwakilishwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Erasto Mhina.

Akizungumza katika Shule ya Sekondari Kwemkabara, wakati wa makabidhiano ya vifaa na vitabu hivyo, alisema kwa sasa wanaamini tatizo la ufaulu wa chini lililokuwa likisababishwa na kukosekana kwa vitu hivyo, litakuwa si kisingizio tena.

Shule hizo ni Bonde Sekondari, Bwembwera, Chief Mang'enya, Kwafungo na Kwemkabara.

Nyingine ni, Magila, Mkurumuzi, Mkuzi, Mlinga, Mlingano, Mtindiro, Muheza High School, Nkumba, Potwe, Shebomeza na Zirai.

Kabla ya makabidhiano hayo, Ofisa Elimu Sekondari Muheza, Serapion Bashange, alisema bado wilaya hiyo inahitaji ufumbuzi kama huo kwa shule nyingine 17.

# Madereva bodaboda 72 mbaroni tuhuma uhalifu

**Na Oscar Assenga,** TANGA


JESHI la Polisi mkoani Tanga, limekamata pikipiki 72 kutokana na makosa mbalimbali, ikiwemo kujihusisha na uhalifu.

Kwenye idadi hiyo pia wapo waliokamatwa wakijihusisha na makosa mbalimbali ikiwemo ya kutokuwa na namba za usajili, kung'oa bomba la kutolea moshi, kutokuwa na leseni na kutovaa kofia ngumu.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi (ACP), Almachius Mchunguzi, alisema waendesha pikipiki hao maarufu kama bodaboda, walikamatwa wakati wa operesheni za kukabiliana na wahalifu.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika tayari majalada yao yamepelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi.

Kamanda Mchunguzi alisema: "Baadhi ya wahalifu hususani watumiaji wa pikipiki maarufu kama bodaboda, wamekuwa wakifahamika lakini wananchi hawatoi ushirikiano kwa kutosha kufanikisha kuwakamata na kuwafikisha mahakamani".





# Utambuzi vipaji kwa watoto watajwa njia kudhibiti ukatili

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

UTAMBUZI wa vipaji vya watoto na kuwapa muda wa kuvifanyia kazi ni moja ya njia muhimu ya kuwaepusha kufanyiwa vitendo vya ukatili na kutumia muda wao kujiimarisha kwenye fani husika.

Kauli hiyo imetolewa na Mtaalamu wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto, Yusuph Mtobela ambaye pia ni Mkurugenzi Shirika la Uzao Wetu linalojishughulisha na ulinzi pamoja na usalama wa mtoto.

Mtobela alitoa kauli hiyo katika mahojiano maalumu na gazeti hili juu ya njia zinazoweza kutumiwa na jamii kuhakikisha vitendo vya ukatili ukiwemo ulawiti, vipigo pamoja na ubakaji vinadhibitiwa.

Alisema katika kutekeleza njia hiyo, shirika lake limeanzisha mradi uitwao 'Kipaji changu, utajiri wangu' unaoendeshwa katika shule zote za msingi na sekondari jijini Mwanza kwa lengo la kuibua vipaji vya watoto walioko shuleni na nyumbani kuanzia umri wa miaka sifuri mpaka 18.

Alisema ili mtoto atambue kipaji chake ni lazima awe na watu wa karibu wa kumwendeleza wakiwemo wazazi na walimu, hali itakayomfanya atumie muda mwingi kwenye kazi hiyo pamoja na vikundi vya watoto wenzake ili kumuongeza ulinzi na usalama.

"Sisi katika kulitambua hili tulianzisha mradi wetu huu wenye miezi mitatu mpaka sasa ukiendeshwa katika shule zote za Serikali na binafsi katika Jiji la Mwanza na shule ambazo tayari zimekubali kushirikiana na sisi ni Sekondari ya Buhongwa, Nyablogoya na Shule ya Msingi Nyasubi.

Alisema kama mzazi hafahamu kipaji cha mtoto basi mzazi huyo kwa sehemu kubwa hafahamu malezi ya mtoto, kwamba mtoto anavyocheza michezo mbalimbali ndio wakati ambao anaonesha kipaji chake.

Hivyo kipaji cha mtoto huanza tangu akiwa tumboni mwa mama yake na asipopewa nafasi ya kukitumia uishia kujiunga na makundi yasiyokuwa na tija.

Kuhusu walimu, Mtobela alisema kama watu wanaokaa na mtoto kwa muda mrefu wakati wa masomo wanatakiwa kumpa msaada mtoto wa katika utambuzi na uendelezaji kipaji chao awapo shuleni na kuacha kuruhusu michezo ya kujificha vichakani.

Alitoa mfano wa aina za vipaji vya watoto kuwa ni pamoja na kundi la "Word smart" linalozalisha vipaji vya watoto wanaoweza kutamka maneno vizuri.

"Kwenye kundi hili tunapata wandishi wa habari, washereheshaji, wahubiri wa kanisani na misikiti, wahariri hivyo kuwaelekeza namna ya kufikia hatua hiyo katika ufasaha ni suala la muhimu," alisema..

Alisema kundi lingine kuwa ni 'Number Smart' linalojikita katika takwimu ambao huzalisha watu wa sayansi na wataalamu wa hisabati pamoja na makundi mengine ya sanaa na muziki.

Mmoja wa wazazi waliopata elimu hiyo, Fraviana Mwantimo alisema atajitahidi kuendelea kuizingatia ili kumkomboa mtoto wake kifikra pamoja na vitendo dhidi ya ukatili.




Balozi wa Ireland nchini, Mary O'Neil (katikati), akiwa pamoja na Reddy Sandewa (kulia) kutoka kampuni ya Kerry Taste & Nutrition na wanachama wengine wa timu ya harambee ya kuchangisha fedha ya St. Patrick iliyodhaminiwa na kampuni ya Kerry na kuandaliwa na Taasisi ya 'Their Lives Matter', jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kwa ajili ya kusaidia watoto wanaopambana na saratani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo waomba kupatiwa leseni zilizofungiwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu na almasi mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kupitia Waziri wa Madini, Antony Mavunde kuwapatia leseni za utafiti na uchimbaji wa madini zilizofutwa ili wazifanyie kazi.

Leseni hizo ni zile zilizofungiwa kutokana na wamiliki wake kushindwa kuziendeleza, hivyo kundi hilo la wachimbaji limeziomba lizifanyie kazi na kuanza kulipa kodi na kunufaika na rasilimali zilizopo.

Walitoa ombi hilo juzi katika mkutano wa kawaida wa Chama cha Wachimbaji Wadogo mkoani Shinyanga(SHIREMA) uliolenga kusikiliza na kupokea maoni ya namna bora ya kuendeleza uchimbaji salama.

Mmoja wa wachimbaji hao kutoka mgodi mdogo wa Ntambalale-Wisolele Kata ya Segese, Juma Saidi alisema hivi karibuni Waziri wa Madini alitangaza kufuta leseni za uchimbaji na utafiti ambazo hajaendelezwa kwa kipindi kirefu na kuomba wapewe kupitia vikundi.

Alisema awali leseni hizo zilikuwa zinasababisha kuibuka kwa migogoro hasa wachimbaji wadogo wanapoyavamia maeneo hayo pasipo kujua na kuendeleza shughuli za uchimbaji.

Mwenyekiti wa SHIREMA Mkoa wa Shinyanga, Hamza Tandiko alishauri serikali kuwapatia leseni wachimbaji wadogo kwenye maeneo waliyoibua ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Joseph Kumburu alisema serikali ipo tayari kutoa leseni hizo lakini ni kwa vikundi vitakavyofuata taratibu. Hivyo aliwataka wale ambao vikundi vyao bado havijasailiwa kuvisajili haraka ili wasiikose fursa hiyo.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba aliwakumbusha wachimbaji wenye leseni wanapotaka kuuza maeneo yao kufuata taratibu na sheria ikiwa ni pamoja na kutangaza na siyo kuuza kinyemela ili kudhibiti migogoro ya mara kwa mara.

# TCDC yaja na 'Move' kurahisisha ufuatiliaji vyama ushirika

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Utafiti na Mafunzo kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Juma Mokili amesema wameanzisha mfumo uitwao 'Move' wenye lengo la kurahisha ufuatiliaji wa vyama vya ushirika nchini.

Aliyasema hayo juzi katika Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika mkoani Shinyanga la mwaka 2024 na kuviagiza vyama vyote vya ushirika kuingia katika mfumo huo haraka ili kupata taarifa za vyama hivyo kwa njia ya kidigitali.

Juma alimwakilisha Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiyege alisema kupitia mfumo huo Mrajisi akihitaji kupata taarifa atazipata kwa wakati.

Licha ya mfumo huo pia alisema kila chama kinatakiwa kuwa na nyenzo au vifaa vyovyote ambavyo vitatumika kwenye mfumo wa TEHAMA ikiwamo tarakanishi, kompyuta mpakato na vishikwambi.

Hivyo alivitaka vyama vya ushirika kuendelea kuzingatia, utekeleza kanuni, sheria na miongozo 15 ya ushirika na kwamba miongozo hiyo bado haijatendewa haki, huku akisisitiza kuandikisha wanachama kwenye mfumo wa 'Move' na watakaofanya vizuri watapewa zawadi.

Mrajisi Msaidizi wa vyama hivyo mkoani Shinyanga, Hilda Boniphace, akielezea hali ya ushirika mkoani hapa alisema vyama vimefikia 273 ambavyo vyote hivyo wamefanikiwa kuvisajili kwenye mfumo wa 'Move' ikiwa ni pamoja na ongezeko la wanachama kutoka 15,400 hadi 72,000.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Shinyanga (SHIRECU), Josephat Limbe, alisema mkakati wa chama hicho katika kumuinua mkulima kiuchumi ni kukarabati kiwanda cha kukamua mafuta kilichopo Mhunze pamoja na Gineri ya Mhunze ya kuchakata pamba.

Mjumbe wa Bodi ya KACU, Emmanuel Nyambi alisema chama hicho kimepata mafanikio mengi ikiwamo kuongeza uzalishaji wa tumbaku.

Alisema pia kuongezwa gharama kutoka Dola za Marekani 1.6 hadi Dola za Marekani mbili, kuongeza wanunuzi wa tumbaku, pamoja na kulipa malipo ya pili kwa wakulima wa pamba.


Ukurasa 12

**Kutoka kupambana na polisi, hadi mjadala mezani, maandamano rafiki**


Ukurasa 13

Falsafa 4R inavyobaki mtaji kusafisha siasa hadi vigingi vya 'ng'ambo ya pili'


# siasa

JUMATANO MACHI 27, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**Mwenyekiti AAFP afunguka yake magumu ya safari zao wanasiasa**

VITA RUSHWA NDANI YA CCM...

# Wadau ndani na nje wampongeza Rais, rai yao akaze kwenye sheria

• Aambiwa akifanikisha, ataweka rekodi...

**Na Sabato Kasika**

MARA zote msamiati rushwa unadumu kupigwa vita katika mustakabali wote kijamii. Hapo ni kuanzia maisha ya kila siku za jamii kwenye nyumba za ibada, mijumuiko ya kijamii, vyama vya siasa, hata serikalini.

Kimsingi, ni imani ya kimataifa katika maadili, sera na sheria za umma ikihimizwa kutokubaliana na tendo hilo la dhuluma ya haki.

Msukumo wa rushwa kwa watu mara nyingi upo katika tabia, mbinu za kununua na kuuza haki, mbadala unaotumika kwa pesa na matendo mengine kama ya ngono.

Rushwa ina kawaida ya kujitokeza penye ushirikiano wa wahusika katika huduma inapotolewa, wakiwa ama na wana tabia hiyo, wenye elimu ndogo ya jambo hilo, pia wakawa na uhitaji.

Tangu uhuru wa nchi serikali imekuwa katika vita kali dhidi yake, serikalini katika jamii na ndani ya chama nchini wakati huo, TANU, ikiongozwa na Rais Julius Nyerere.

Ni aina ya msimamo waliodumu nao Chama Cha Mapinduzi (CCM), mrithi wa TANU ndani ya mfumo wa serikali yake awali iliyokuwa na Taasisi ya Kuzuia Rushwa (PCB), kabla ya kuboreshwa kuwa jeshi pana mwaka 2007 katika serikali ya awamu ya tano, ilipoanzishwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), yenye ofisi sasa kila wilaya.

Hadi sasa CCM inaendelea kudumisha itikadi hiyo ya kukabili rushwa ndani ya chama, katika sehemu ya msimamo wake endelevu.

**ZAMA AWAMU SITA**

Uongozi wa CCM katika kuliendeleza hilo, wakati wa kura za maoni kuelekea uchaguzi, hakuna kada atakayepita kwa mbinu chafu bali atachaguliwa kulingana na utendaji wake ndani ya eneo analowakilisha.

Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akatoa maelekezo kwa wawakilishi wake wakiwamo madiwani na wabunge, hawatakiwi kuonekana kugawa ishara za rushwa, hasa vilivyozoeleka; khanga, vitenge na hata fedha.

Dk. Samia anatamka kwamba wanapotoa vitu hivyo, ni wazi kwamba hawajafanya kazi katika maeneo wanayowakilisha, pia ni sawa na kuhonga, ili wachaguliwe tena.

Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia akatumia fursa hiyo, kutoa maelekezo kwa makada, kwamba atawapima katika uchaguzi ndani ya chama kwa kazi zao wanavyowajibika katika ubunge na uwakilishi waliotumikia.

Ilikuwa katika hafla ya kufungua tawi la CCM la Chaani Masingini, Mkoa wa Kaskazini Unguja, akitamka katika lugha ya kuwaonya makada wa chama hicho kwamba

"Ninataka kuwaambia jambo! Tutakapopimana katika uchaguzi ndani ya chama chetu, tutapimana kwa kazi za wabunge na wawakilishi walizofanya."

Ni kauli inayobeba ujumbe wa kunyoosha kidole, akisisitiza kuwa kazi za kuwaletea wananchi maendeleo ndizo zitawabeba wagombea wa CCM katika uchaguzi mkuu ujao na si njia nyingine na kwamba wajiandae


Mwenyekiti wa CCM, Rais Dk. Samia Suluhu. **PICHA: MTANDAO**

nalo.

Hapo akaendelea:"Si khanga na vitenge. Kama ni zawadi, zitolewe katika sherehe zikiwamo sikukuu za kidini, si kusubiri wakati wa uchaguzi unakaribia ndio mgombea aanze kutoa."

Ni tamko la kuwajibika katika vita dhidi ya rushwa, chama tawala kikiendesha vita hivyo kuanzia ndani ya mfumo wake kupata wawakilishi wasafi wa ubunge na udiwani.

Hapo ndio sehemu muhimu inayomwibulia Rais viongozi wasaidizi wake watarajiwa, wakiwamo mawaziri, meya na wenyeviti katika halmashauri, iwapo wao na chama chao watashinda katika uchaguzi mkuu ujao, wakapewa nafasi ya kuunda serikali na timu ya Baraza la Mawaziri.

**WANENAVYO WADAU SIASA**

Baada ya tangazo hilo, Nipashe imezungumza na wadau wa siasa kupata maoni kuhusu vita dhidi ya rushwa ndani ya chama hicho, hasa kutokana na kuwapo tuhuma za vitendo hivyo, zikisababisha malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanachama.

Thomas Ngawaiya, kada wa CCM aliyewahi kutumikia nafasi za juu katika vyama vya NCCR - Mageuzi na TLP, anayekiri kuwapo baadhi ya wagombea ndani ya chama wanaojihusisha na rushwa, hata kusababisha kura za maoni kurudiwa.

Ngawaiya anasema: "Nikupe mfano mdogo tu kwamba uchaguzi uliopita wa viongozi ndani ya chama, ilibidi aliyekuwa Katibu Mkuu, Daniel Chongolo (sasa Mkuu wa Mkoa Songwe), kufuta uchaguzi na kuelekea kurudia upya,".

Sasa anashauri hatua, watakaobainika kujihusisha na rushwa, watajwe hadharani, hata wengine wenye nia ya namna hiyo waogope akikumbusha kuwa ni kosa la jinai.

"Njia ya kuikomesha ni mwenyekiti kupenyeza vikosi vyake viwanase wahusika na kuwataja hadharani, ili wengine waogope kuumbuka," anasema Ngawaiya.

Kada huyo anashauri mchakato wa kuwabaini watoaji rushwa usisubiri uchaguzi, bali ufanyike mapema kudhibiti wanaoendelea na tabia hiyo, kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, pia

INAENDELEA UK. 14




Maandamano ya chama cha siasa, CHADEMA, baada ya kufunguliwa ulingo wa demokrasia ya vyama nchini. **PICHA: MTANDAO**

# Kutoka kupambana na polisi, hadi mjadala mezani, maandamano rafiki

## • Sauti upinzani, AZAKI zaiwajibisha serikali - CCM

**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

Ni swali wakirushiwa wachambuzi wa mambo, wanaelezea iko katika ukweli kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anaelewa vyema umuhimu wa demokrasia, haki na uhuru wa kutoa maoni.

Hilo sasa linampa uhakika kuwapo maridhiano, kusameheana na kutumikia pamoja kwa ajili ya maendeleo ya nchi na kufanikisha ajenda ya kuwaletea wananchi maisha bora.

Katika demokrasia hiyo, chama tawala kinakumbushwa kuhusu uwajibikaji kupitia sauti zinazopazwa na vyama vya upinzani na raia mmoja mmoja, hatimaye kujirekebisha na kufanya vizuri zaidi kwa manufaa ya umma.

Leo hii, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anaafiki kuwa anakotoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), kina nafasi ya kufanya kiufanisi zaidi kupitia hoja zinapoibuliwa na vyama vya upinzani, asasi za kiraia 'AZAKI' na wananchi wakinufaika kwa kujiimarisha.

Hiyo inatajwa ni katika kuzifanyia kazi na hatimaye kuendelea kuongoza kwa kutumia mipango na mikakati yake, ushauri, kukosolewa kunakotolewa na wengine na hivyo kutatua kero za wananchi.

Mnamo Januari mwaka jana, Rais Dk. Samia akizungumza na viongozi wakuu wa vyama vya siasa vya upinzani anaandika historia, pale alipotangaza kufuta zuio na kuurejesha uhuru kwa 'wafungwa vyama vya kisiasa.'

Hiyo ni kwa namna ya kuruhusu mikutano ya hadhara isiyo na bughudha. Akiwa Ikulu jijini Dar es Salaam Rais Dk. Samia akasema: "Nianze na la mikutano ya hadhara, hii ni haki kwa sheria zetu.

> Lakini kama waungwana wastaarabu niwaombe tunatoa ruhusa ya vyama vya siasa twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, za kupevuka, za kujenga na si kubomoa, kurudi nyuma.

"Ni haki ya vyama kufanya mikutano yao na kwa bahati taarifa zote mbili zimeigusa kuwa ni jambo muhimu sana. Uwapo wangu leo mbele yenu ni kuja kufanya ruhusa, kuja kutangaza lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka."

**UHAI WA VYAMA**

Ikumbukwe kuwa uhai wa vyama vya siasa ni pamoja na kuendesha shughuli zake za kisiasa kila siku ambapo mikutano ya hadhara, kupokea wanachama, kunadi sera zake ni jukwaa muhimu la kupanua na kuendeleza wigo mijini na vijijini.

Ndiko kwenye tafsiri ya kuzungumzia masuala muhimu ya kitaifa, pia mtu mmoja mmoja na hata kimataifa, ili kutafuta majibu ya pamoja kwa ustawi na maendeleo ya wananchi.

Kutokana na zuio lililokuwepo, lilikwamisha vyama vya siasa kufanya shughuli zake kwa uhuru, na ndiyo maana Rais Dk. Samia akaondoa kifungo hicho ili kutoa uwanja sawa wa siasa za ushindani kati ya chama tawala na vyama vya upinzani na sasa hadithi za kukatazwa mikutano zimesahaulika.

Hatua hiyo inayoondoa zuio la mikutano ya kisiasa, imeweka mazingira wezeshi ya kuufanya uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, hata uchaguzi mkuu wa mwakani 2025, pia wa serikali ya mitaa unaotarajiwa mwaka huu.

Sababu hapo inatajwa ni kuviwezesha vyama vyote vilivyopewa fursa sawa za kunadi sera zao kwa wananchi, na yule mwenye hoja za kuvutia wapigakura zinazogusa maisha yao, apate fursa ya kuwatumikia kupitia sanduku la kura.

Mara kadhaa, Rais Samia amejitangaza ni muumini wa kukosolewa, hivyo vyama vya upinzani viikosoe serikali kikamilifu kwa kutumia lugha za staha na kwa kuheshimu mila, desturi, sheria, kanuni na miongozo ya nchi kwani kukosolewa kunaipa serikali nafasi ya kujua changamoto zilizopo kwa ajili ya kuzifanyia kazi.

Katika mkutano na viongozi wa vyama vya upinzani, Rais Samia akawaambia: "Wajibu wenu ni kufuata sheria zinavyosema, kanuni zinavyoelekeza ndiyo wajibu wenu.

"Lakini kama waungwana wastaarabu niwaombe tunatoa ruhusa ya vyama vya siasa twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, za kupevuka, za kujenga na si kubomoa, kurudi nyuma."

Aidha, vyama vimepata uwanja sawa wa kufanya siasa za ushindani kwa kutekeleza kwa vitendo haki ya kuandamana ili kufikisha ujumbe mbalimbali

Hapo, mathalan unatolewa mfano wa kuwapo maandamano ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo -CHADEMA, kinachoandamana katika matukio ya majiji mbalimbali nchini hivi karibuni; Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha na kinaendeleza kikishinikiza hoja zake.

Ni maandamano yanayobeba madai kuwapo hali bora kutokana na ugumu wa maisha na kupinga sheria za uchaguzi zilizofanyiwa marekebisho hivi karibuni na bunge.

CHADEMA kote imefikisha ujumbe kwa serikali bila bughudha na mlinzi wa amani na mali za rais, Jeshi la Polisi likiilinda mikutano hiyo kikamilifu.

Vilevile, kukawapo uhuru wa kujieleza, kwa wananchi na kwa wanasiasa kwa ujumla ni nyenzo muhimu katika uwanja wa demokrasia na kufikia maendeleo, ndivyo anavyoamini Rais Dk. Samia.

Uhuru wa kujieleza na kukosoa umepewa msukumo mkubwa na serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia kwani ni katika kujieleza na kukosoa kistaarabu na kiungwana, ndiko kunapotoka mawazo mazuri ya kujenga.

Ndiko kunakoonyesha wapi ilikosea, na namna bora zaidi ya kuinua uchumi, jamii na siasa. Wananchi wote, waliosoma na wasiosoma, wanayo mawazo muhimu ambayo kama yakisikika na kufanyiwa kazi, yatachangia maendeleo ya nchi kwa kasi kubwa na pia kiufanisi.

Aidha, inafafanuliwa, Mama amewapa uhuru, wanachama na viongozi wa vyama vya siasa kwa kuwahakikishia kuwa milango iko wazi wakati na muda wowote kushauri na kutoa maoni na mawazo yao ili serikali iweze kufanyia kazi kwa manufaa ya taifa.

Eneo lingine analopewa 'maua yake' Rais Dk. Samia ni katika mazingira wezeshi ya siasa za ushindani kupitia falsafa yake '4R' yaani'; Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga upya.

Kimsingi, wanasiasa wanapokuwa wameridhiana kwa pamoja na kuondoa vikwazo vilivyokuwa vikiathiri mshikamano na umoja wao, huwa dhahiri ushindani utafanyika vyema.

Ndiko anakokanyagia Rais Dk. Samia, mara kadhaa akifanya vikao na viongozi wa vyama vya siasa ili kujenga maridhiano, huku ustahimilivu ukihitajika sana katika kusubiria hoja zilizotolewa kufanyiwa kazi na serikali.

Hilo linaendana na mageuzi katika sheria mbalimbali yanayofanyika, kufanikisha azma ya serikali kujenga upya nchi kufikia maendeleo endelevu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

***• Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma: Simu: +255 0620 800 462.***

# Falsafa 4R inavyobaki mtaji kusafisha siasa hadi vigingi vya 'ng'ambo ya pili'

• Ilianza kwa kunadiwa, kisha sasa inatekelezwa

Na Gaudensia Mngumi

KWENYE moja ya kampeni za uchaguzi mkuu, mgombea anaahidi kujenga daraja na kuapa kwa miungu yote kuwa kama halitajengwa akatwe kidole gumba.

Baada ya miaka mitano, anarudi tena kuomba kuchaguliwa aongoze jimbo. Anashangaa kukutana na mabango yenye mapanga na visu.

Hakukumbuka alichoahidi hadi aliposoma 'tunakukata kidole liko wapi daraja letu?'

Ndiyo mfano wa ahadi hewa, wagombea au watiania wanazowahadaa wapigakura ili wawachague kwenye uongozi.

Ni ujumbe kwa wanasiasa wanaotangaza nia ya kuwania uongozi iwe kwenye serikali za mitaa au ubunge ama udiwani na urais kwenye chaguzi zinazoanza mwaka huu.

Wanaonywa na Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake, inayoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Mtandao wa Wanawake na Katiba kwa udhamini wa Mfuko wa Udhamini wa Wanawake (WFT-T).

Ilani inaangazia uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu wa 2025.

Ilani inawaonya wanaotoa ahadi hewa kuwa wanaozitoa hawana kipya cha kuwafanyia wananchi badala yake wanawadanganya.

Aidha, inawataka wapigakura kuwa makini na wagombea hao na kuwataka waonyeshe nia na njia za dhati za kuleta usawa wa kijinsia na kuyapa kipaumbele masuala kama ukatili na ubaguzi wa kijinsia na namna watakavyoyaondoa.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongozwa na aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, wakiingia ndani ya ukumbi wa Bunge, kwa ajili ya kulihutubia tarehe 22 Aprili, 2021 Jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

### UJUMBE WA VYAMA

Vyama vya siasa vinatajwa na ilani kuwa ni walinzi wa lango kuu la kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi na kwenye nafasi za uongozi kitaifa, hivyo inazidai mengi taasisi hizo.

Mosi, inavitaka kuchukua hatua za kuchagua na kuteua viongozi ndani ya vyama ili kutoa fursa kwa wanachama wanawake kushiriki katika uongozi na uamuzi ndani ya chama.

Aidha, vizingatie misingi iliyobainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda, katiba ya Tanzania na dira ya 2025 kuhusu usawa wa kijinsia kwenye uongozi ndani ya vyama hivyo.

Kadhalika vyama vijielimishe kuhusu faida za kuzingatia usawa wa jinsia katika uongozi na maamuzi ndani ya taasisi hizo ili kuujua umuhimu wa kuleta mabadiliko katika mfumo wa uongozi ndani ya taasisi hizo.

Halikadhalika, vyama hivyo vitenge mafungu maalumu kuwawezesha wanawake vijana kushiriki katika uongozi, lakini viache malumbano ya ubinafsi badala yake vijenge hoja na utamaduni wa majadiliano ya kistaarabu yasiyo na vitisho au vitendo vya kuwadhalilisha wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Pia inavitaka vionyeshe nia ya kupambana na ufisadi na rushwa za aina zote ikiwamo ya ngono kwa wagombea wanawake na ukatili wa kingono dhidi yao.

Ilani inavionya viache kutumia viti maalumu kushawishi wanawake kujiondoa kwenye nafasi za kushindana majimboni, jambo linalosababisha kuwatumia kuwapigia debe wanaume wanaowania nafasi hizo.

"Wanawake wanachama wa vyama vya siasa watambue kwamba wanapochaguliwa kwa mfumo wa 'viti maalumu' hawana fursa sawa za ushiriki. Hawawezi kuteuliwa kwenye nafasi ya Waziri Mkuu au katika mabaraza ya mikoa," inaonya ilani.

Inaeleza kuwa walioingia kwa mfumo wa viti maalumu hubaguliwa katika uteuzi wa wenye viti wa kamati mbalimbali hata kama sheria hazikatazi.

Kadhalika, hawapati fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo zinazowawezesha wabunge waliochaguliwa kwa kura majimboni kuendelea kujiimarisha kwenye uchaguzi.

### HAWATAUNGA MKONO

Kwa kauli zao ndani ya ilani wanawake, wanasema hawataunga mkono chama kisichoonyesha nia ya kubomoa mfumo dume na mifumo kandamizi ndani ya vyama.

Mifumo hiyo inajidhihirisha kwenye safu za uongozi ndani ya vyama na ile ya waliojitolea kuwania nafasi kwenye chaguzi za serikali na mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025.

"Chama chenye uongozi unaodhalilisha wanawake katika ngazi yoyote kuanzia kwenye kaya, hakitaungwa mkono. Hata vyama au chama chenye historia ya kufuja mali za taifa na kujilimbikizia mali kwa njia zisizo halali."

Vilevile hakuna kuunga mkono vyama visivyoonyesha utayari wa kimkakati wa kufungua milango ili wanawake washiriki kikamilifu ndani ya vyama vyao na katika kuwania uongozi wakati wa uchaguzi.

"Sisi wanamtandao wa wanawake, katiba, uongozi na uchaguzi pamoja na mitandao mingine ya tapo (movement) la ukombozi wa wanawake kwa sauti moja tunakiri tutaunga mkono vyama vilivyoteua wagombea katika nafasi mbalimbali ambao kwa maoni yetu ni wagombea wenye kuheshimu utu wa wanawake.

Wasio na tamaa ya kuhodhi mamlaka, walio tayari kusimamia na kuweka mbele maslahi ya taifa ili rasilimali au utajiri wa Tanzania unatumika kwa manufaa ya wote."

> Wagombea ambao hawana historia ya ufujaji, wizi na hata kashfa za ngono na udhalilishaji wowote wa kijinsia, wataungwa mkono pia.

Aidha, inasema wagombea ambao hawana historia ya ufujaji, wizi na hata kashfa za ngono na udhalilishaji wowote wa kijinsia, wataungwa mkono pia.

### KUNUNUA KURA

Ilani inasema katika chaguzi zilizopita wanaharakati wapigakura walishuhudia wagombea wasio na sifa wakihaha kutumia uwezo wao kifedha kununua kura.

Inamfananisha kiongozi huyo na sumu kwa taifa, maendeleo ya demokrasia na hata kwa harakati zinazolenga kuwakomboa wanawake na makundi yaliyo pembezoni yanayotaabika kutokana na rasilimali za taifa kutowafikia.

"Vile vile tulishuhudia wagombea wakitumia lugha ya kuwadhalilisha wagombea wengine hasa wanawake. Kwa umoja wetu tunasema anayetumia lugha ya kudhalilisha utu wa mwanamke amefilisika kimawazo tena asiyestahili kura zetu."

Ilani inawaonya wagombea wasitumie nguvu ya fedha kununua kura bali busara na nguvu ya hoja kushawishi wapigakura. Pia mgombea au mpigadebe anatakiwa ajiepushe na kutumia matusi au ubabe kudhalilisha wanawake wagombea.

### ASASI ZA KIRAIA

Ilani inaeleza kuwa katika ilani zilizopita asasi nyingi za kiraia zimejihusisha na elimu ya mpigakura ikiwa ni pamoja na kuhamasisha kupigakura, kuwachagua viongozi bora na waadilifu.

Aidha, elimu ya wapigakura imetolewa siku chache kabla ya uchaguzi na haikuwa endelevu kuna asasi chache sana zilizowekeza kwenye kutetea na kuhamasisha jamii kuhimiza wanawake wenye uwezo kujitokeza zipo chache zilizowezesha kwa njia ya elimu na zilizoendeleza elimu ya wapigakura kwa muda mrefu ni chache.

Ilani inaeleza kuwa kasoro hiyo inaathiri uelewa wa wapigakura kuhusu kanuni, taratibu na haki na wajibu wao katika uchaguzi wa viongozi.

Inazitaka kuunganisha nguvu ya pamoja katika kuhamasisha wanawake wenye uwezo kugombea nafasi za uongozi kukataa kuburuzwa kama wapigadebe na kupinga kurubuniwa na nafasi za upendeleo zinazotumia kama kigezo kikuu cha kupeleka mwanamke kwenye uongozi iwe bungeni au halmashauri.

Aidha, AZAKI zinatakiwa zitoe elimu endelevu kwa wapigakura inayozingatia masuala ya haki za wanawake katika uongozi kitaifa kama sehemu muhimu ya kuendeleza demokrasia shirikishi, pia zionyeshe kwa vitendo imani thabiti isiyobagua wanawake na makundi mengine kwenye uchaguzi.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Mwenyekiti AAFP afunguka yake magumu ya safari zao wanasiasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HUYO ni Mwenyekiti wa chama cha AAFP, Said Soud Saidi anayeisimulia Nipashe hali ya vipindi vya kabla na baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, namna vyama vya siasa vilipitia magumu.

Hiyo anasema ni hata nchi ikaonekana kuwa na vyama vya siasa katika umaarufu wa majina zaidi, kuliko nafasi kama za kuikosoa, kuishauri au kuielekeza serikali.

Anasema, ni hali iliyoifanya jamii kukosa watetezi na wananchi kukosa nguvu kazi ya vyama vyao vya siasa, huku mustakabali wa demokrasia na utawala bora ukawa mgumu.

Hapo anataja mabadiliko ya sasa anayataja kuwa mageuzi pale, Rais anajishughulikia na mageuzi ya katiba, kuwanyooshea Watanzania demokrasia yao.

Anafafanua kuwa, suala la katiba ndilo lenye manufaa zaidi kijamii, akionyesha ndio msingi pekee anaoamini unawafanya Watanzania kupata haki zao za msingi.

Mwenyekiti huyo anasema licha ya Rais Samia kuruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara na maandamano, bado ana kikwazo cha kwamba vyama vya siasa havijapata ruzuku kama katiba inavyoelekeza.

Anasisitiza ulazima wa suala hilo la vyama kuwezesha kupata asilimia zilizotajwa za mapato ya serikali kugawa na hatimae vyama vikapata ruzuku na kuingia katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 vikiwa vinajitambua.

"Vyama havina ruzuku, vimeshindwa kutanua demokrasia na sasa tunaweza tukafikia mahali vyama vikafa vyenyewe, kwa sababu uwezo wa kujiendesha unashindikana," anasema.



Mwenyekiti wa Chama cha AAFP, Said Soud. **PICHA: MTANDAO**

**AMSIFU DK. SAMIA**

Soud anarejea chama chake AAFP kwamba kinapongeza uongozi huo wa miaka mitatu wa Rais Dk. Samia katika uongozi, kwani awali walikutana na chamgamoto nyingi zilizokwaza kiutendaji katika.

Katika hilo, anasema wanaamini katika uwezeshaji na walipambana kucahngia nchi kuelekea kwenye maendeleo makubwa kiuchumi.

Anafafanua kisiasa, amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuchangia kuiweka nchi katika hali nzuri ya maelewano na mshikamano, kwa sababu alikuwa yupo tayari kuzungumza na vyama vya siasa katika kujenga hoja ya amani na utulivu kupatikane mafanikio katika mazungumzo hayo.

Mwenyekiti huyo anasema, licha ya kuwapo changamoto nyingi, lakini wanakabiliana nazo wakizifanyia kazi.

Kuhusu hali ya uchumi, Soud anasema nchi imekuwa katika mazingira ya maendeleo, licha ya kwamba wananchi maisha yao hayajawa mazuri kwa sababu ndani ya Tanzania zaidi ya wananchi milioni 16, wanaishi katika maisha duni, wakiohitaji kuinuliwa kimaisha kumudu milo mitatu kwa siku.

"Bado Rais Samia anakabiliwa na kazi ya kuinua maisha ya watu, licha ya kwamba serikali inatangaza uchumi umekuwa lakini bado maisha ya watu hayajakuwa.

"Ni kwa sababu wananchi ndio wenye uwezo mkubwa wa kufanya nchi kuwa na uchumi au kutokuwa na uchumi, muhimu wananchi kupata maisha mazuri, fedha za matumizi, matibabu na elimu," anasema.

Anfafanua kuwa Rais Dk. Samia ana safari bado ya kuirudishia heshima Tanzania katika mazingira yanayoendelea, akiamini endapo atafanikiwa kuiongoza tena nchi katika miaka mitano ijayo, anaweza kufanikiwa kwa asilimia 95.5 katika maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Soud anamtaja Rais Dk. Samia katika uongozi wake hana ubaguzi, huku akibashiria kukiwapo katiba inayopigiwa upatu sasa, itazidi kuwalinda wanawake, uhuru na haki zao hata wanakuwa bna uwezo wa kutumikia taifa na kupata maendeleo.

"Kama katiba itakuwa hii ambayo bado inautata wa kumtambua kiongozi hawezi mwanamke kufanikiwa, mwisho wataogopa hata kugombea, kwa sababu matokeo yake baada ya kuhesabiwa kura zinapigwa mafungu bila ya kuhesabiwa na hatimaye kutangazwa," anasema.

Anahitimisha kwa kujadili hali ya demokrasia nchini, kwamba utataa wake unajitokeza kupitia katiba wanayoipigania ipatikane mpya, akilalamika iliyoko sasa haijawa na muongozo sahihi wa haki za Tume ya Uchaguzi, haki za mgombea, haki za mwanamke na haki za kiongozi.

## Wadau ndani na nje wampongeza Rais, rai yao akaze kwenye sheria

**INATOKA UK. 11**

"Nimuombe mwenyekiti wa CCM Taifa asirudi nyuma katika uamuzi huu alioutangaza, ili kulinda heshima ya chama. Ana vyombo vingi vya kunusa kila kona, avitumie kuwabaini watu wa aina hiyo," anasema.

Ngawaiya anafafanua madhara ya rushwa kwenye uchaguzi, ikiwamo kupata viongozi ambao si chaguo la wapigakura, hivyo hawawezi kusaidia maendeleo yao.

"Raha ya uongozi mtu achaguliwe kihalali, atashirikiana na wananchi kupanga mipango ya maendeleo, aliyeingia madarakani kwa rushwa, atahangaika kurudisha fedha alizohonga kupata uongozi," anasema.

Anawakumbusha mantiki ya Rais Dk. Samia, kila mgombea ashinde kihalali na sio njia ya mkato isiyo na tija kwa maendeleo ya nchi, hivyo anapaswa kusaidiwa na viongozi wenzake katika vita hiyo, kupatikane waliochaguliwa kihalali.

**TAKRIMA IFUTWE**

Kada wa chama cha upinzani, NCCR-Mageuzi, Joseph Selesini, aliyekwishawahi kuwa mbunge kwa tiketi ya Chadema, anasema mbinu itakayosaidia kuondoka rushwa ndani ya CCM, ni kufuta sheria iliyoruhusu kuwapo kwa 'takrima'.

Selasini anasema ni sheria iliyochangia kuenea rushwa, huku akifafanua:"Kwanza nimpongeze mwenyekiti wa CCM kwa ujasiri huo ... kumaliza rushwa ndani ya chama chake, afute sheria iliweka takrima."

Anasema baadhi ya wanasiasa wanatumia vibaya takrima, wamegeuza kuwa uchochoro wa kufanya mambo yanayohusiana na rushwa kwa kisingizio kuwa wanatoa 'takrima'.

Mwanasiasa huyo anasema takrima imesababisha kuwapo udalali wa uongozi na anafafanua kuwa, baadhi ya watumishi badala ya kufanya kazi, wanahangaika kutafuta pesa za kuhonga wapate uongozi katika siasa.

"Unakuta mtu ananunua fulana, kofia, khanga, vitenge, mipira na vitu vingine vingi na kuvigawa jimbo zima...," anasema, akishauri Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wanatakiwa kuziba mianya yote ya rushwa mapema, ili kusaidia taifa kuwa na viongozi wanaotokana na ridhaa ya wananchi.

"Mama Dk. Samia ameanza vizuri!. Hili tatizo la rushwa limeshika mizizi na ni mtambuka. Nimpongeze tena kwa hatua hii, najua litamletea msuguano kwenye chama chake na nje ya chama.

"Akifaulu atakuwa ameandika historia na huenda kwa mara ya kwanza tukawa na viongozi wanaotokana na ridhaa ya wananchi."

MIFUMO IBADILISHWE

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Dk. Ananilea Nkya, anasema rushwa haiko CCM pekee, bali imetapakaa kote kivyama, na kwamba njia ya kuimaliza ni kubadilisha mifumo ya sasa inayohusiana na sheria za kukabili rushwa.

"Serikali unaweza kupeleka miswada bungeni ipitishwe kuwa sheria kali za kupambana na rushwa, kwani kwa sasa hali si shwari ndani ya nje ya vyama. Watu wanatoa na kupokea rushwa," anasema Dk. Ananilea, ambaye ni mwanahabari.

Mwenyekiti huyo wa zamani wa Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), anasema hatua hiyo ya kuwa na mifumo mipya ya kukabiliana na rushwa, inaweza kukomesha vitendo vyake, vinavyojitokeza kwenye kampeni za uchaguzi na maeneo mengine.

"Ushauri wangu kwa Rais ni huo! Nadhani wote tunapaswa kumuunga mkono kutokana na hatua hiyo ya kuweka wazi msimamo wake dhidi ya rushwa, hivyo wapinga rushwa wote tuungane naye," anasema.

Anaeleza imani yake kwamba, sheria kali ndio mwiba dhidi ya watoaji na wapokeaji rushwa na anaongeza kuwa serikali ione ukubwa wa tatizo na kuweka sheria ambazo wahusika wataogopa kujihusisha na vitendo hivyo.





## TARURA yamwagiwa sifa uboreshaji miundombinu Singida

**Na Elisante John,** SINGIDA

BAADHI ya wananchi mkoani Singida wamepongeza juhudi za Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) kwa kuboresha miundombinu ya barabara katika Manispaa ya Singida.

Uboreshaji huo ni pamoja na kujenga barabara kwa kiwango cha lami, hivyo kupunguza adha kwa shughuli za usafirishaji abiria na uchukuzi wa mizigo.

Wakizungumza baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Mwenge-Mungumaji na ile ya Imbele-Mnung'una, kwa kiwango cha lami, wakisema itarahisisha mawasiliano katika Mji wa Singida,

Mmoja wa wakazi hao, Devota alisema kukamilika kwa miundombinu hiyo kutarahisiaha shughuli za uchukuzi wa mizigo na usafirishaji abiria kwa haraka zaidi.

Mkazi mwingine, Said Athuman, alisema kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Imbele-Mnung'una, itaongeza kasi ya uchukuzi wa abiria na biashara ya usafirishaji wa abiria kupitia usafiri wa bajaji na bodaboda mkoani Singida.

Akizungumza ujenzi wa miundombinu hiyo, Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Ibrahim Kibasa, alisema wamedhamiria kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha uchukuzi wa mizigo na usafirishaji abiria kwa uhakika wakati wote.

Kibasa alisema katika kuhakikisha miundombinu hiyo inapitika wakati wote, serikali imetekeleza miradi hiyo kati ya Julai mwaka jana hadi Februari mwaka huu, lakini akaiomba jamii kushiriki katika kuzitunza barabara hizo ili ziweze kudumu zaidi.

Kwa mujibu wa Kibasa, TARURA Mkoa wa Singida, unahudumia mtandao wa barabara wa kilometa 533, ndani ya Manispaa ya Singida, huku utekelezaji wa ujenzi wa miradi yake mbalimbali, ikiwa imefikia asilimia 75 ya miradi yote.

# Hoja 15 za muungano zatatuliwa miaka mitatu ya Rais Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amesema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan hoja 15 za muungano zimetatuliwa.

Alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya muungano.

Alisema hadi kufikia mwaka huu jumla ya hoja za muungano ambazo zimefanyiwa kazi ni 22 na zilizobakia ni hoja nne ambazo bado juhudi zinaendelea ili kuzimaliza.

"Hadi mwaka 2020 hoja za muungano ambazo zilikuwa zimetatuliwa ni hoja saba, lakini katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia tumeweza kutatua hoja 15 zaidi ya nusu na kufanya zibakie hoja nne ili tumalize zote" alisema Jafo.

Aidha, aliwataka Watanzania kuendele kuenzi na kuulinda muungano wa Tanzania na Zanzibar wakati huu ambapo unafikisha miaka 60.

"Miaka 60 siyo jambo dogo sana ni umri wa mtu mzima wengi wenu hapa mlikuwa bado hamjazaliwa hivyo tunapaswa kuulinda kwa hali na mali kwani wenzetu wengi wamejaribu lakini walishindwa sisi ni nchi pekee katika Afrika ambao tumefanikiwa kuwa na muungano kwa miaka yote hiyo" alisisitiza Jafo.

Aidha, alisema mafanikio mengine yaliyopatikana katika miaka 60 ya muungano ni pamoja na jamii kuendelea kuwa tulivu na yenye amani ukilinganisha na mataifa mengine.

"Lakini pia kama taifa ndani ya miaka 60 tumefanikiwa kuwa na maendeleo makubwa katika sekya ya afya, elimu na miundombinu ya barabara ambapo karibu nchi nzima imeunganishwa na lami kasoro M koa wa Kigoma tuu ambao nao pia tupo katika juhudi kubwa za kufanikisha kwani zipo kandarasi zinaendele sasa" alisema.

Kadhalika, alimshuru Rais Samia kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kuulinda muungano huo kwa kusaidia miradi mbalimbali katika pande zote mbili za muungano.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema kuelekea miaka 60 ya muungano ofisi yake imeandaa utaratibu wa viongozi wa wizara zenye idara za muungano kueleza mafanikio yaliyopatikana.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan 'Zungu' kwa niaba ya Spika wa Bunge, akiongoza kikao cha Kamati ya Uongozi na Bajeti katika mashauriano kuhusu mambo ya muhimu yaliyojitokeza kwenye kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Dk. Biteko: Upungufu watumishi afya, ustawi wa jamii ni 52%

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko amesema upungufu wa watumishi wa kada za afya, ustawi wa jamii na lishe na vifaa tiba unakadiriwa kufikia asilimia 52 kutokana na ongezeko la vituo vya kutolea huduma katika ngazi ya afya ya msingi.

Amesema kutokana na hali hiyo serikali imetaja imekuja na suluhisho la kukabiliana na upungufu huo ikiwamo kuajiri watumishi kulingana na bajeti.

Aliyasema hayo jijini hapa wakati wa mkutano wa kwanza wa kimataifa wa afya ya msingi uliokwenda sambamba na uzinduzi wa namba 115 ya Mfumo wa Usafiri wa Dharura kwa Wajawazito, waliojifungua na Watoto Wachanga (M-MAMA).

Dk. Biteko alisema kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 nafasi za ajira 18,528 zimetolewa katika mamlaka za serikali za mitaa, kwamba ajira hizo zimeleta mabadiliko makubwa katika utoaji huduma.

"Ninatambua idadi hii haiwezi kukidhi mahitaji yote, serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ili kupunguza changamoto hiyo. Moja ya mikakati ni kuendelea kutoa vibali vya ajira kulingana na uwezo wa bajeti ya serikali,"alisema.

Aidha, alisema kila mwaka kinamama zaidi ya milioni 2.3 na kati yao 45,000 wanapata dharura zinazohitaji usafiri.

"Tangu kurasimisha kwa mfumo zaidi ya dharura 60,000 zimesafirishwa na kwa sasa kwa rufaa zinazotolewa kituo kwa kituo tunapata dharura zaidi ya 5,500 kila mwezi ikiwa ni sawa na dharura 200 kila siku na dharura nane kila saa nchini," alisema.

Naibu Waziri, Ofisini ya Rais, TAMISEMI, Dk.Festo Dugange, alisema Serikali imejenga na kuimarisha miundombinu ya afya msingi, kuajiri watumishi na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi.

Alisema hadi kufikia Februari mwaka 2024, sekta ya afya ya msingi nchini ina vituo vya kutolea huduma za afya 6,933 zikiwamo zahanati 5,887 vituo vya afya 874 na Hospitali za Halmashauri 172.

"Takwimu hizi zinaonyesha kwamba kuna ongezeko kubwa la vituo katika afya ya msingi ikilinganishwa na idadi ya vituo 5,270 katika mwaka 2015. Hii ni hatua kubwa katika kuelekea kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote nchini," alisema.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza idadi ya vituo vya afya ya msingi, alisema kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali za afya, ustawi wa jamii na lishe na vifaa tiba mbalimbali.

Hivyo, alimuomba Rais Samia kuendelea kutoa kibali cha ajira kwa watumishi wa kada za mbalimbali za afya, ustawi wa jamii, na lishe, huku akiomba mashirika ya kimataifa, wadau wa maendeleo na sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika eneo hilo muhimu ili kupata ufumbuzi wa kudumu.





# TTB yaanza uhamasishaji utalii wa kiutamaduni kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) imeanza kuhamasisha utalii wa kiutamaduni katika mikoa ya kusini, ili kuwavutia watalii kujifunza tamaduni za wakazi wa mikoa hiyo na kuongeza pato la wananchi na Taifa.

Hamasa hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Utalii Kusini (REGROW) ambapo bodi hiyo imeanza kuhamasisha kwa kutoa mafunzo maalumu kwa waongoza watalii ili wawe wanawapeleka watalii kwenye vivutio hivyo.

Ofisa Utalii wa TTB, George Mwagane alisema wanatoa mafunzo hayo kwa vikundi 10 vya waongoza watalii kutoka katika mikoa minne ya Morogoro, Iringa, Mbeya na Ruvuma ili watumike kuhamasisha watalii kutembelea vivutio hivyo.

Alisema vikundi hivyo vya kiutamaduni vimekuwa vikitumia shughuli zao zikiwemo ngoma za asili kama bidhaa na hivyo watalii wakitembelea watakuwa maeneo hayo watakuwa wanajifunza tamaduni na kulipia ili wapate burudani.

Alisema watalii wakitembelea maeneo hayo mbali na kujifunza pia wataongeza siku za kuishi katika maeneo hayo ili kuongeza kipato cha wakazi wa maeneo husika kwa kununua bidhaa mbalimbali zinazozalishwa kwenye maeneo husika.

"Lakini pia hii itasaidia kuongeza ajira kwa vijana hawa ambao wanaongoza watalii na itasaidia pia kuzalisha ajira ambazo sio za moja kwa moja, kwahiyo tunaamini kwamba utalii huu ni muhimu kwa maendeleo ya sekta hii," alisema Mwagane.

Ofisa wa TTB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Hoza Umbula alisema aina ya utalii huo ni miongoni mwa vivutio vipya ambavyo awali vilikuwa havihamasishwi miaka ya nyuma na kwamba kwa sasa wamebaini kuwa ni muhimu kuhamasisha.

Alisema watalii watakaokuwa wanavutiwa na aina hiyo ya utalii mbali na kufurahia utalii huo pia watajifunza vyakula na shughuli zingine za kiutamaduni ambazo zinafanywa na jamii husika.

Alisema vivutio hivyo ni vingi katika mikoa ya kusini mwa Tanzania na kwamba mradi huo wa REGROW utasaidia kuviibua na kutembelewa kwa kiwango kikubwa na watalii.

"Hawa waongoza watalii ambao tunawapatia mafunzo haya watatusaidia kuwafikisha watalii kwenye maeneo haya, watalii watanunua bidhaa mbalimbali za kiutamaduni ambazo zinazalishwa na wananchi," alisema Umbula.

Baadhi ya viongozi wa vikundi ambavyo vilihudhuria mafunzo hayo walisema watahakikisha wanawafikisha watalii kwenye maeneo yote ambayo yana vivutio hivyo ili wajifunze vitu mbalimbali vya kiutamaduni.

Mmoja wa waongoza watalii hao, Joseph Ndomondo kutoka mkoani Ruvuma, alisema miaka ya nyuma sekta ya utalii ilikuwa imewekewa mkazo katika mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania na mikoa ya Kusini ilikuwa haikumbukwi.

Alisema kwa sasa mbali na bodi ya utalii kuhamasisha lakini pia serikali imeboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji hali ambayo inawafanya watalii kuvifikia vivutio vilivyopo kiutalii.

Alisema elimu ambayo wameipata itawasaidia kuwaongoza watalii kwenye maeneo yenye vivutio, ili kuifanya sekta hiyo kukua katika ukanda huo.

Mwishoni mwa mwaka 2023, maofisa wa Bodi ya Utalii walifanya ziara maalumu ya kuhamasisha utalii Kusini mwa Tanzania kwa kutembelea vivutio mbalimbali.

## Shule kongwe 3 zapewa msaada mifuko 400 ya saruji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson kupitia taasisi yake ya Tulia Trust, amekabidhi mifuko 400 ya saruji kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa katika shule kongwe tatu za Jiji hilo.

Akikabidhi mifuko hiyo, Ofisa Habari wa taasisi hiyo, Joshua Mwakanolo alisema mifuko 200 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja katika Shule ya Msingi Mlimani iliyoko katika Kata ya Sinde.

Alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba 13 vya madarasa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi na hivyo waliamua kujenga vyumba hivyo ili kupunguza tatizo.

Alisema mifuko mingine 100 inapelekwa katika Shule ya Wasichana ya Dk. Tulia iliyopo Kata ya Iyunga na mingine 100 inapelekwa katika Shule ya Sekondari Itende.

Alisema: "Lengo la kufanya ukarabati wa madarasa haya ni kuwasaidia watoto hawa kutobanana kwenye vyumba vichache vilivyopo, lakini pia mbunge ameamua kukarabati madarasa kwenye shule hizi kongwe".

**Akikabidhi mifuko hiyo, Ofisa Habari wa taasisi hiyo, Joshua Mwakanolo alisema mifuko 200 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja katika Shule ya Msingi Mlimani iliyoko katika Kata ya Sinde.**



Maofisa wa Taasisi ya Tulia Trust (wenye fulana nyeusi), wakimkabidhi Diwani wa Kata ya Sinde, jijini Mbeya, Fanuel Kyanula (wa pili kushoto), mifuko 200 ya saruji, iliyotolewa na taasisi hiyo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Mlimani, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# DC aagiza kukamatwa wanafunzi wanaozurura

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa amewaagiza watendaji wa kata, mitaa na vijiji wilayani hapa kuwakamata wanafunzi ambao wanazurura mitaani wakati wa masomo, ili kukabiliana na tatizo la utoro pamoja na ukatili wa kijinsia.

Agizo hilo alilitoa wakati wa kikao cha wadau wa elimu cha Halmashauri ya Mji Njombe kilichoenda sambamba na utoaji tuzo kwa shule zilizofanya vizuri kitaaluma kilichofanyika mkoani hapa.

"Mtoto atakayeonekana anazagaa wakati wa masomo achukuliwe, atafutwe mzazi wake na mzazi wake awajibishwe na jamii husika kwa sababu haiwezekani watoto tukawapoteza, watoto kwenye utoro wanafanyiwa vitu vibaya sana kuna mambo mengi yanatokea huko mtaani lazima tuwalinde watoto wetu," alisema Kasongwa.

Hata hivo alisema kuwa kila kata na mitaa zinapaswa kutengeneza mkakati wa kuwalinda watoto na kutaka jambo hilo kufanyika kwa haraka kwa sababu ya kuonekana kuna wimbi kubwa la watoto mitaani.

"Mimi mwenyewe nitamchukulia hatua Mtendaji wa Kata wa eneo hilo kwa maana ya kusema hivyo ningeomba sana watendaji wa kata, mitaa na vijiji washirikiane na walimu wakuu la sivyo itakuwa jambo ambalo si shirikishi," alisema Kasongwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthum Sadick aliwataka walimu kuzingatia uweredi na kuacha kufanya vitendo vizivyofaa kwa wanafunzi.

"Walimu badala ya kuwa ni wazazi tunajisaau tunakengeuka, tumekuwa na kesi nyingi za walimu kufanya ambavyo sivyo kwa watoto kwa hiyo niwaombe walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari kwamba ambaye mnamuona anatabia ambayo ni mbaya mchukulieni hatua," alisema Sadick.

Awali Ofisa Elimu Taaluma Msingi Halmashauri ya Mji Njombe, Bryson Kingililwe alisema zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu na hivyo kushindwa kufikia malengo yalizokusidiwa.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni upungufu mkubwa wa miundombinu ya madarasa, matundu ya vyoo, utawala, maktaba na nyumba za walimu.

"Kwa upande wa uhaba wa nyumba za walimu hasa ukizingatia shule nyingi zimejengwa maeneo yasiyo na makazi ya watu ambako nyumba za kupanga hazipo hata zikipatikana hazina ubora hii hufanya walimu kutokuwa na mazingira ya kufanya kazi kwa ufanisi," alisema Kingililwe.

Baadhi ya wakuu wa shule za serikali akiwemo Mkuu wa Shule ya Sekondari Yakobi, Deogratias Msagati alisema moja ya sababu iliyosababisha shule yake kufanya vizuri kitaaluma ni pamoja na kukutana na wazazi na kuwaeleza kuhusu umuhimu wa kushiriki malezi kwa watoto.



## Jaji Mkuu: Mashindano ya Qur'ani yanaimarisha dini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla amesema uwepo wa mashindano ya Qur'ani ni muhimu kwa mustakbali wa kukuza na kuimarisha dini ya kiislamu.

Jaji Khamis aliyasema hayo jana katika mashindano ya kuhifadhi Qur'ani kwa wanafunzi wa madrasa za Mkoa wa Kusini Unguja yaliyofanyika katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein Tunguu mkoani humo.

Alisema kuwa jambo hilo ni muhimu kutokana na kuwa Qur'ani ndiyo kitabu kinachotowa mwongozo mzima wa dini ya kiislamu na maisha ya mwanadamu kwa ujumla.

Hata hivyo alisema kuwa katika mashindano hayo amejionea uimara wa vijana wanavyojiamini na kuweza kusimama mbele za watu na kuisoma vizuri.

Aidha, alisema kuwa lengo la tamasha hilo ni kurudisha utamaduni wa kiislamu kwa kuwaweka watu pamoja katika mwezi mtukufu wa Ramadhan ambalo linahusisha shughuli mbalimbali mbali ikiwemo kuwakutanisha na kubadilishana Mawazo.

Alisema kuwepo kwa tamasha hilo ni jambo jema na kuwaomba viongozi wa dini na wananchi kulisimamia jambo hilo hasa katika mwezi huu wa Ramadhan ambao ndio ilipoteremshwa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kuwa anadhamira ya dhati kupitia mashindano hayo kuibua vipaji katika ngazi za mkoa vitakavyoshiriki kitaifa na kimataifa ili kuwawakilisha vyema katika ngazi zinazofuata.

Aidha alisema wataendeleza jambo hilo la kheri kwa miaka yote lengo ikiwa ni kuhuisha na kuendeleza dini yao na kuendeleza imani ya dini kwa wananchi wa mkoa huo.

# Makamu wa Rais akemea tabia wizi mitandao ya simu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah amesema baadhi ya watumiaji wa mitandao ya simu hawana uelewa, kwamba kuna mambo yanayofanyika katika mitandao yenye viashiria vya wizi.

Aliyasema hayo juzi visiwani Zanzibar baada ya futari iliyoandaliwa na kampuni ya simu ya Tigo- Zantel na kuitaka kampuni hiyo kushirikiana na mamlaka zingine kuwadhibiti watu hao wasiendelee kuwaibia wananchi, kutofanya mambo yasiostahiki ndani ya nchi.

"Wapo watu huwatumia ujumbe watumiaji wa simu kwamba wamepokea shilingi milioni moja, sasa katika hali ya kawaida ukiona ujumbe kama huo wa kuingiziwa fedha anaona ni jambo la kawaida, kumbe ni ujanja tu hakuna fedha iliyotumwa" alisema Hemed.

Aliitaka kampuni hiyo kudhibiti mambo hayo, kutafuta namna ya kuzuwia na wale wote wanaohusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Alisema isingekuwa jambo la faraja kampuni hiyo kutumika kwa kutuma ujumbe usio leta picha nzuri, kwamba utasababisha kuleta dosari kwa kampuni.

Aidha, aliwataka wale wote watakaojihusisha na wizi wa mitandaoni wachukuliwe hatua za kisheria kwa kushirikiana na mamlaka zingine za kiserikali.

"Lakini hili likitokea kwa watendaji wenu maana mambo haya kama mtu siyo mtaalamu hawezi kulifanya, hivyo ikitokea kwa kampuni yenu naomba mchukue hatua kali sana ili kukomesha mtendaji mwingine asiweze kuyafanya haya" alisema Hemed.

Alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano ili kufanya kazi iliyokusudiwa na kutimiza matakwa ya wananchi hasa katika eneo la mawasiliano.

Hemed alisema kuimarika kwa huduma za mawasiliano ya simu kwa asilimia 97 yatarahisisha na kuimarika kwa sekta ya uwekezaji na kuifanya Zanzibar kuwa Kituo cha Uwekezaji Ukanda wa Afrika yaMmashariki.

Alisema kampuni ya Tigo-Zantel imefanikiwa kufikisha huduma za mawasiliano kwa asilimia 97 katika maeneo yote ikiwemo ya vijijini, ambapo sekta ya uwekezaji imechukuwa nafasi kubwa.

Alisema hali hiyo inaleta matumaini na kwenda sambamba na dhamira ya Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi kukiunganisha kisiwa cha Zanzibar na mawasiliano ya simu na huduma nyingine za mawasiliano.

Hata hivyo alisema serikali imepata faraja kutokana na kazi inayofanywa na kampuni hiyo ambapo awali wananchi wengi walikuwa na wasiwasi na hofu kufuatia kampuni hizo kuunganisha nguvu zao za pamoja katika kufanya kazi.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa kampuni ya Tigo-Zantel, Innosent Rwetabura alisema kampuni hiyo inatambua umuhimu wa mwezi wa Ramadhan ambao ni nguzo muhimu mwenye imani, mwezi wa kuvuna baraka na kuwaweka watu pamoja na ndiyo maana wameandaa chakula hicho cha pamoja na wateja wao.

Alisema mwezi huo pia ni ukumbusho wa ushirikiano na kupata hisia mtu ambae ameshinda na njaa na kupata fursa ya umuhimu wa familia na jamii katika kusaidiana na kudumisha mshikamano.

Aidha, alisema kampuni hiyo imewekeza katika kuboresha miundombinu ya teknolojia ya mtandao huo na imekuwa kampuni ya kwanza ya mawasiliano Tanzania kwa kuweka kasi ya mawasilaino ya 5G visiwani Zanzibar.




Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah akishiriki futari iliyoandaliwa na kampuni ya Tigo Zantel, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaanza ujenzi barabara za vijijini Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kazi ya ujenzi wa barabara za vijijini katika Kisiwa cha Pemba (km115) umeanza na kwamba utarahisisha huduma za usafiri pamoja na kuimarisha sekta ya kilimo.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk.Khalid Salum Mohamed alipotembelea Barabara ya Wingwi Mapofu hadi Tumbe Bandarini (km 5) Kisiwani Pemba.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha miundombinu ya Kisiwa cha Pemba inaimarishwa katika kiwango cha ujenzi wa lami.

Alisema kazi hiyo imeanza, itaelekea hadi katika maeneo ya sekta ya utalii pamoja na maeneo huru ya uchumi Micheweni kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji.

Dk. Khalid alisema serikali imejipanga kutangaza sekta ya utalii katika Kisiwa cha Pemba kupitia majengo ya kale yaliyobeba historia kubwa, huku kazi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ambao utakifunguwa kisiwa hicho umeanza.

Hivyo, aliwataka makandarasi wa kampuni ya IRIS kujipanga vizuri kuhakikisha wanatekeleza mradi huo kwa mafanikio na kuhakikisha adhma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga miundombinu ya barabara hadi vijijini katika Kisiwa cha Pemba inatimia.

"Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi tumeanza kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara za vijijini ambazo unatekelezwa na kampuni ya IRIS kutoka Uturuki, matarajio yetu makubwa ni kufanyika kazi hiyo kwa mafanikio makubwa kwa kuzingatia viwango" alisema.

Mkandarasi wa kampuni ya IRIS, Yussuf Aguas alisema wamejipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara hizo kwa ufanisi na kuzingatia viwango na ubora wa kazi.

Alisema wameanza ujenzi huo kwa Barabara ya Wingwi Mapofu inayoelekea katika Bandari ya Tumbe (km 5).

"Tunao uhakika wa kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara za Pemba zinazokwenda vijijini na hiyo ni kutokana na uwezo wetu wa kujenga barabara katika sehemu mbali mbali duniani" alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Khatib Mbarouk, alisema ujenzi wa barabara za vijijini ni muhimu, ndiyo zitakazokifunguwa Kisiwa cha Pemba na kukiunganisha na miundombinu ya barabara.

Alisema vipo baadhi ya vijiji katika Mkoa wa Kaskazini havijaunganishwa na barabara za lami na hivyo kufanya mawasiliano ya usafiri kuwa magumu.

Aidha, alisema ujenzi wa barabara za ndani utasaidia wakulima ikiwemo wa karafuu kufikisha bidhaa zao hadi mjini kwa urahisi pamoja na wavuvi kufikisha samaki wao sokoni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBERT CHARLES BUGAISA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba **T 383 CYR,** CHASSIS NAMBA **NCP600203557** na ENGINE NAMBA: **2NZ3505715.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **9910840445315**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PRISCA HENJEWELE MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T176CZS** aina ya Nissan DUALIS, Chassis No. **NJ10006343,** Engine No. MR20269718A. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/8186/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**PASCAL TADEI MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 880 AEA – TOYOTA HIACE, T 880 DFZ – TOYOTA COASTER na T 456 BDT – CANTER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/45223/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA TRACTOR

**HAROUB SEIF SULEIMAN** anatangaza kupotea kwa kadi za tractor **FORD na MASSEY FERGUSON** zenye usajili namba **T 770 DBV na T 767 DBV.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/TAN/2518/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**HAROUB SEIF SULEIMAN** anatangaza kupotea kwa kadi za magari NISSAN SAFARI na CARAVAN zenye usajili namba **T 544 AFW na T 183 AGC.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/TAN/2515/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ROMAN JOACHIM ASSENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 356 ABT – BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/46842/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ONESPHORY DOMINICK MTUNDU** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **T 956 CBS, T 270 CCQ, MC 328 APD.** Yeyota atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/2514/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ONESPHORY DOMINICK MTUNDU** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 354 ACP, MC 874 BMQ, MC 924** BMQ. Yeyota atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/2518/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ONESPHORY DOMINICK MTUNDU** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 200 AZB, T 491 CHW, MC 572 BAR.** Yeyota atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/2516/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**MEENDA GEORGE MALLYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CARINA** yenye usajili namba **T 908 ABD , CHASSIS NAMBA: ST176025280** na **ENGINE NAMBA: 3E0560555**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi Polisi taarifa *PHQ/DAR/KIN/46721/2024* na kadi ya gari aina ya **HINO RANGER** yenye namba ya usajili **T 435 AZD ,** CHASSIS NAMBA: **FC2JCA12757** na ENGINE NAMBA: **J08CB26801,** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa: **PHQ/DAR/KIN/46703/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**ROMANUS EZEKIA KADUMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya trekta yenye namba za usajili **T 128 APR** aina ya **FORD,** Chassis No. **312223,** Engine No. **312223**. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/8373/2024.**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE COURT OF DISTRICT COURT OF KONDOA AT KONDOA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5259 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late MARK KUNDA KIVANGWA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PETRONILA MARK KUNDA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of The Probate Rules Gn 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 04, 2024
Dated at Kondoa this 14 Day of 03, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**

**WILAYA YA MOROGORO, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...14/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JOSEPH JOHN wa K/NDEGE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JOHN JOSEPH MNYUNE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 05 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 03 mwaka 2024**

**HAKIMU**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Faye aahidi kuitawala Senegal kwa unyenyekevu

**DAKAR,** Senegal

MGOMBEA wa upinzani Senegal Bassirou Faye anajiandaa kuwa rais baada ya mpinzani wake mkuu kutoka chama tawala kukubali kushindwa, kufuatia uchaguzi uliofanyika juzi, huku akiahidi kutawala taifa hilo kwa unyenyekevu.

Ni mara ya kwanza katika uchaguzi wa 12 wa urais zilizofanyika chini ya haki ya upigaji kura wa watu wote tangu Senegal ilipopata uhuru kutoka kwa Ufaransa mwaka wa 1960 ambako mgombea wa upinzani ameshinda katika duru ya kwanza ya upigaji kura.

Mpinzani wake mkuu kutoka muungano unaotawala, Amadou Ba, mwenye umri wa miaka 62, aliutambua ushindi wa Faye na kumpigia simu kumpa salamu za pongezi.

Rais anayeondoka Macky Sall, ambaye hakugombea baada ya ushindi wake wa 2012 na 2019, pia alimpongeza, akisifia kile alichokielezea kuwa ni ushindi wa demokrasia ya Senegal.

Katika hotuba yake ya kwanza baada ya uchaguzi, Faye aliwaambia waandishi wa habari kuwa katika kumchagua yeye, watu wa Senegal wameamua kuachana na yaliyopita, akiahidi utawala wa uwazi.

Aidha, alimshukuru Rais Macky Sall na wagombea wengine kwa kuheshimu utamaduni wa demokrasia wa Senegal kwa kutambua ushindi wake mapema kabisa kabla ya matokeo rasmi kutolewa.

Ilielezwa kuwa hatua ya aliyekuwa mgombea wa uraisi wa upinzani Ousmane Sonko kumuidhinisha naibu wake huyo wa zamani Faye kabla ya uchaguzi wa Jumapili ilikuwa muhimu.

Sonko, alishitakiwa kwa uasi mwezi Julai na kuzuiwa kugombea katika uchaguzi ili kumrithi Rais Macky Sall, hatua iliyomlazimu kumchagua Faye kama mbadala wake.

"Chaguo langu la Faye sio chaguo kutoka moyoni, bali la hoja. Nilimchagua kwa sababu anatimiza vigezo ambavyo nimeviweka. Ni mchapakazi na amesoma katika shule ya kifahari kabisa nchini Senegal," alisema.

"Hakuna anayeweza kusema sio mwaminifu. Naweza hata kusema kuwa ni mwaminifu zaidi kuliko mimi. Ninamkabidhi mradi huu mikononi mwake," alisema Sonko.

Aidha, tume ya uchaguzi ilisema matokeo ya awali yalionyesha Faye akiwa na karibu asilimia 53.7 ya kura na Amadou Ba akiwa na asilimia 36.2 kwa kuzingatia hesabu kutoka asilimia 90 ya vituo vya kupigia kura katika duru ya kwanza ya uchaguzi.

Hata hivyo, ilieleza kuwa matokeo rasmi yanatarajiwa kutangazwa ifikapo mwishoni mwa wiki hii. **DW**



Rais mteule, Bassirou Faye wa chama cha upinzani akihutubia wananchi Senegal. **PICHA: MTANDAO**

## Uhaba fedha kuviondoa vikosi vya SADC Msumbiji

**MAPUTO,** Msumbiji

VIKOSI vya Wanajeshi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambao walitumwa kukabiliana na waasi wa Kiislamu nchini Msumbiji wanatarajiwa kuondoka nchini humo kutokana na matatizo ya kifedha.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Msumbiji Veronica Macamo, alisema hayo yanajiri kwa sababu SADC imekuwa ikizingatia ukomo wa bajeti yake.

Veronica akieleza kuwa umoja huo unaamini kuwa Msumbiji iko shwari ikilinganishwa na mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambayo imekuwa ikikabiliwa na makundi yenye silaha kwa miongo kadhaa.

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, alisema SADC inapanga kuondoa vikosi vyake ifikapo Julai, mwaka huu. Akieleza kuwa hatua hiyo haimaanishi kwamba vita vya kitaifa dhidi ya makundi ya kijihadi vitakoma.

"Nchi pia zimejitolea kufanya kazi nasi kwa pande mbili, ikiwa ni sawa, kama Wasumbiji tunahitaji kuwa tayari kwa ukweli huu. Tusikengeushwe, jukumu kubwa liko kwetu," alisema.

Ilielezwa kuwa kundi la waasi lililojihami lilishambulia eneo la kaskazini mwa Msumbiji kwa miaka sita, huku kundi la Islamic State likisema ndilo lililohusika na baadhi ya ghasia hizo.

Uasi huo, ambao umehusisha mashambulizi kadhaa dhidi ya umma na vikosi vya jeshi, ulisababisha majibu ya kijeshi Julai 2021.

Usaidizi ulikuja kwanza kutoka kwa Rwanda, ambayo ilituma zaidi ya wanajeshi 2,000 nchini Msumbiji, na kisha kutoka SADC. **BBC**

# eGA: TEHAMA italeta ufanisi utendaji serikalini

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba, amesema wataendelea kusimamia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini ili kuleta tija na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Ndomba ameeleza hayo baada ya hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan kueleza kuwa viongozi wa umma wanapaswa kufahamu na kutumia mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) iliyoko serikalini katika utekelezaji wa majukumu yao.

Rais Samia aliagiza viongozi hao kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Mawasiliano wa e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo.

Akizungumza kuhusu matumizi ya mifumo ya TEHAMA serikalini, Mkurugenzi Mkuu Ndomba alisema e-GA itaendelea kusimamia matumizi ya TEHAMA serikalini ili kurahisisha upatikanaji huduma bora kwa wananchi kwa wakati mahali walipo.

"Moja ya maeneo ambayo Rais Samia amekuwa akiyapa kipaumbele ni kuimarisha Serikali Mtandao kwa kuhakikisha taasisi za umma zinatumia TEHAMA kwenye utendaji kazi wake na wananchi wanapata huduma za serikali kidijitali mahali popote na muda wote.

"Katika kuhakikisha tunafikia lengo la Rais, e-GA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma tumetengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo imesaidia kupunguza gharama, kuokoa muda, kuongeza ufanisi na kurahisishia wananchi kupata huduma kidijitali mahali walipo," alisema.

Ndomba alisema mfumo wa e-Mrejesho unawezesha wananchi kutuma kero au malalamiko, maoni, maswali na pongezi kidijitali kwenda katika taasisi yoyote ya umma na kisha kupata mrejesho wa utekelezaji wake kidijitali mahali walipo.

Pia alisema unasaidia kuokoa muda na fedha, kwani mwananchi halazimiki tena kusafiri umbali mrefu kwenda katika ofisi ya umma kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko yake au kufuatilia utekelezaji wake na badala yake, anaweza kufanya hivyo kidijitali kupitia simu yake ya kiganjani mahali alipo.

"Zamani ilikuwa mtu akihitaji kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma inayotolewa na taasisi ya umma ilimlazimu kufika katika taasisi hiyo na kuwasilisha malalamiko yake kwenye sanduku la maoni au kuwasilisha barua katika taasisi hiyo na kisha kufanya ufuatiliaji utekelezaji wake, lakini kwa sasa anaweza kuwasilisha maoni hayo kidijitali," alifafanua Ndomba.

Akiwaapisha wateule wake hivi karibuni, Rais Samia aliwataka kutumia mfumo wa e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi na kutoa mrejesho kwa wananchi pamoja na serikali kuhusu utekelezaji maoni hayo.

# WIZARA, DRUM BEATS KUENDESHA TAMASHA KITAIFA LA UTAMADUNI

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Kampuni ya Drum Beats Carnival (T) Limited ya jijini Dar es Salaam, zimesaini makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya kuratibu Tamasha la Kitaifa la Utamaduni lililopangwa kufanyika Agosti 25, mwaka huu, mkoani Ruvuma.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana katika ofisi za wizara zilizopo eneo la Mtumba jijini Dodoma kati ya Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Nicholas Mkapa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Drum Beats Carnival (T) Limited, Selestine Mwesigwa.

Akizungumza baada ya utiaji saini, Mkapa alisema Wizara ina matarajio makubwa kutoka kwa Drum Beats katika kuendesha tamasha hilo ambalo ndio kubwa la kitamaduni Tanzania na kuongeza kuwa huo ni mwanzo mzuri wa kushirikiana na sekta binafsi katika kuendesha matamasha ya wizara hiyo.

**Mbali na hilo alisema tamasha hilo litasaidia pia kupanua wigo kwa wadau wa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa matukio ya kijamii.**

"Hii haina maana kuwa serikali imeliachia tamasha hili moja kwa moja bali tunatoa fursa kwa sekta binafsi itoe mchango wake na pia kuhakikisha tamasha hili linafanyika kitaalamu zaidi na linakuwa kubwa, lakini serikali itaendelea kusimamia kwa karibu," alisema.

Mkapa alitoa wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi katika hatua zote za tamasha hilo kuanzia awali hadi ngazi ya kitaifa kwani ni la kitaifa linalolenga kuimarisha utamaduni wa Tanzania.

Mkurugenzi wa Utamaduni wa wizara hiyo, Dk. Mnata Resani, alisema tamasha hilo la kitamaduni la kitaifa litafanyika Songea mkoani Ruvuma kuanzia Agosti 25 hadi 28, mwaka huu, huku akisisitiza kuwa ujio wa Drum Beats kushirikiana na wizara ni dalili njema kuwa tukio hilo litakuwa katika viwango vya juu zaidi.

"Kutakuwa na mambo mbalimbali kama vile vyakula vya kitanzania, zana mbalimbali, mavazi na pia kutakuwa na maonyesho barabarani yaani street carnival," alisema na kuongeza kuwa serikali itafanya kazi kubwa ya kutoa hamasa ili watu wengi zaidi washiriki katika tukio hili kubwa.

Kwa upande wa Afisa Mtendaji Mkuu wa Drum Beats Carnival (T) Limited, Mwesigwa, alisema kampuni yake iko tayari kushirikiana na wizara kuhakikisha tamasha hilo linafanikiwa.

"Timu yetu imekamilika na tuko tayari kushirikiana na wizara kuhakikisha malengo yanafikiwa na pengine kuvukwa," alisema.

Alisema baada ya utiaji saini, kampuni yake itatoa ratiba nzima ya shughuli zote za tamasha hilo. "Tunatoa wito kwa Watanzania kutuunga mkono ili kufanikisha jambo hili," alisema.

# Uhamiaji FC yapania kucheza michuano CAF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kurejeshwa madarakani kwa mara nyingine, uongozi wa Klabu ya Uhamiaji, umesema malengo yao makubwa kwa miaka hii mitatu ni kuhakikisha timu hiyo inapata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Klabu ya Uhamiaji wiki wiki iliyopita ilifanya uchaguzi mkuu na kuwarejesha viongozi wake madarakani ambapo kwa mujibu wa katiba yao kila baada ya miaka miatatu inawataka kufanya uchaguzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Salehe Abasi, amabaye kwa mara nyingine amerejea katika nafasi hiyo, alisema miaka mitatu iliyopita ambayo walichaguliwa walitimiza lengo lao kubwa moja likiwa ni kuipandisha timu hiyo kucheza Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema miaka mitatu hii ambayo wamerudi tena madarakani wanataka kutimiza lengo lao la kuhakikisha timu hiyo inashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho Afrika, michuano ambayo huandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF. Alisema katika kuhakikisha hilo linatimia, wanaweka mkazo zaidi katika michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufui FA Cup, ambayo wamefanikiwa kutinga hatua ya 16-bora.

Mbali na kushiriki mashindano ya kimataifa, lakini pia alisema wanataka kuendesha timu hiyo kwa njia ya kisasa zaidi 'kidigital' kama zilivyo klabu nyingine kubwa.

"Sasa hivi timu zinaendeshwa 'kidigital' zaidi, kutumia mitandao ya kijamii ambayo ndio inawafuasi wengi na inasababisha timu kufuatiliwa na kujulikana, huu nao ni mpango mwingine ambao utasaidia katika kuitangaza timu na hata kupata mechi nyingi za kirafiki,"alisema.

Hata hivyo, aliwataka wanachama wa timu hiyo kushirikiana pamoja kwa kila hatua ili kuhakikisha wanatimiza mipango waliyokusudia kuifanya.

**NIPO FITI...**



Mdhamiru Yassin akifanya mazoezi juzi usiku baada ya kujiunga na timu yake ya Simba akitokea Azerbaijan kwenye majukumu ya timu ya taifa, na jana kikosi hicho kilirejea jijini Dar es Salaam tayari kwa mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri, itakayopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# Kocha mpya Tabora Utd afunguka mazito

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Tabora United, Denis Goavec, amesema baada ya muda mfupi tu kuwapo ndani ya kikosi hicho, amegundua mambo kadhaa ambayo anadhani yalikuwa yakisababisha timu hiyo isifanye vizuri katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo raia wa Ufaransa aliyechukua nafasi ya Mserbia, Goran Copunovic, alisema hakukuwa na nidhamu kwa wachezaji, ambapo pia hawakuwa na furaha kikosini.

"Nilichokutana nacho kwanza kabisa nidhamu kwa wachezaji ilikuwa ndogo, halafu walikuwa hawana furaha, siwezi kujua ni kwa sababu gani ilikuwa hivyo kabla ya sisi kufika.

"Kazi yangu kubwa iliyopo kwa sasa ni kurudisha nidhamu na furaha kwa wachezaji, kama hivyo vyote vikiwapo basi kila kitu kinawezekana," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa anakiandaa kikosi chake kwa ajili ya mechi ya Kombe la FA itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Aprili 4, mwaka huu, dhidi ya Singida Fountain Gate.

"Itakuwa mechi nzuri kwetu, hatutokuwa tayari kushindwa na ndiyo mechi itakayorejesha furaha ya mashabiki wa Tabora United," alisema Goavec.

Timu hiyo inashika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 21, ikicheza mechi 21, kushinda nne, sare tisa na kupoteza nane.

Awali, mara tu baada ya kupewa timu, kocha huyo alidai kugundua shida kwenye safu yake ya ushambuliaji pamoja na viungo watengeneza nafasi.

"Nimeangalia kitu na nimegundua safu ya ushambuliaji ina shida, tumetengeneza nafasi chache na tumefunga mabao machache, kwa hivyo lazima kwanza tuanze na yale mapungufu makubwa ambayo nimeyagundua baada ya kufuatilia mechi kadhaa ilizocheza huko nyuma," alisema kocha huyo.

Timu hiyo imefunga mabao 15 mpaka sasa na kuruhusu 25, ikiwa imesalia na mechi tisa tu za Ligi Kuu msimu huu.

**Itakuwa mechi nzuri kwetu, hatutokuwa tayari kushindwa na ndiyo mechi itakayorejesha furaha ya mashabiki wa Tabora United.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FRANK ATAKIWA UNITED**

KABU ya Manchester United inamlenga kocha wa Brentford, Thomas Frank, kuchukua mikoba ya Erik ten Hag pale Old Trafford msimu wa majira ya joto, na sio kocha wa England, Gareth Southgate. ***(Football Transfers)***

**WERNER KUFUNGWA SPURS**

TOTTENHAM Hotspur wanania ya kukamilisha mkataba wa kudumu kwa mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28, lakini wanaripotiwa kuwa hawana haraka ya kuanzisha kipengele cha kumnunua kwa pauni milioni 14.5. ***(Four Four Two)***

**DIOMANDE KUTUA ARSENAL**

ARSENAL imefikia ofa ya pauni milioni 51 pamoja na bonasi ambayo Chelsea wametoa kwa Sporting Lisbon kwa mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande, 20. ***(Record)***

**HAALAND NA FURSA MADRID**

MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23, anaitazama robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya Manchester City dhidi ya Real Madrid kama fursa ya kuthibitisha uwezo wake wa kuhamia miamba hao wa Hispania. ***(AS - kwa Kihispania)***

**BENRAHMA KUSAINI LYON**

KLABU ya West Ham inatarajia winga wa Algeria mwenye umri wa miaka 28, Said Benrahma kusaini mkataba wa kudumu katika klabu ya Ligue 1 ya Lyon msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**ATAJWA LEVERKUSEN**

BAYERN Leverkusen ni miongoni mwa klabu za juu za Ulaya zinazotaka kumsajili mlinda lango wa Everton na England, Douglas Lukjanciks, 16. ***(Mail)***

**ZERBI HANA HARAKA**

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, amefurahishwa na nia ya Bayern Munich kutaka huduma yake - lakini kocha huyo wa Italia hana haraka ya kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake wa muda mrefu. ***(Mirror)***

**CHELSEA KUADHIBIWA**

CHELSEA inakabiliwa na adhabu ikiwa ni pamoja na kukatwa pointi kwenye Ligi Kuu England iwapo itapatikana na hatia ya kukiuka sheria za matumizi chini ya umiliki wa Roman Abramovich. ***(Guardian)***

**CHIESA AGOMBEWA EPL**

LIVERPOOL itachuana na Manchester United kumnunua fowadi wa Juventus raia wa Italia, Federico Chiesa, 26. ***(Teamtalk)***

**TOULOUSE KUNUNULIWA**

WAMILIKI wa Liverpool, Fenway Sports Group na Mkuu mpya wa Soka, Michael Edwards, wanachunguza mpango wa kununua Klabu ya Toulouse Kuu ya Ufaransa. ***(Football Insider)***

## DO... ZA SOKA MAG... YA ULAYA




# DE JONG HAONDOKI BARCELONA - LAPORTA

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesisitiza kuwa kiungo Frenkie de Jong hana nia ya kuondoka klabuni hapo kwenye dirisha linalokuja la usajili wa majira ya kiangazi.

**De Jong amekuwa mchezaji muhimu kwa Barca tangu uhamisho wake wa euro milioni 75 kutoka Ajax mwaka 2019.**

Lakini thamani yake kubwa imekuwa ikimfanya kuwa mtaji licha ya matatizo makubwa ya kifedha ya klabu hiyo na Barca walijaribu kumbakiza Mholanzi huyo ambaye awali alikuwa akiwaniwa na Manchester United karibu miaka miwili iliyopita.

Licha ya Wakatalunya wakiwa bado hawajaondoka kwenye hali mbaya ya kifedha, mustakabali wa De Jong - na wale wengine kadhaa akiwamo Ronald Araujo na Pedri - bado haujajulikana, ingawa mchezaji mwenyewe amekuwa akisisitiza kwamba anataka kubaki na Laporta amethibitisha kwamba bado haijabadilika.

**●●● Tuna nafasi ya mkataba mpya, tumefurahishwa naye, kama mtu anataka kuondoka...**

"Ana furaha akiwa Barcelona. Kitu cha mwisho ambacho angetaka ni kuondoka Barcelona. Ameniambia zaidi ya mara moja, kwamba amefurahishwa hapa," alisema rais huyo akiliambia gazeti la Mundo Deportivo.

"Tuna nafasi ya mkataba mpya. Tumefurahishwa naye," aliongeza Laporta.

"Sina wasiwasi na mtu yeyote na kama mtu anataka kuondoka, hatuwezi kwenda kinyume na matakwa ya mchezaji. Lakini nadhani kila mtu anataka kubaki na tunataka kila mmoja wetu abaki."

Manchester United waliendelea kumtaka De Jong, ambaye alikuja kujulikana Ajax chini ya Erik ten Hag, majira ya joto yaliyopita, wakati Bayern Munich pia waliuliza wakati huo.

Amekuwa akihusishwa mara kwa mara na Paris Saint-Germain, huku tetesi za Chelsea pia zikiibuka tena hivi karibuni.

Mkataba wa De Jong huko Barcelona, uliotiwa saini mwaka 2020, utaendelea hadi mwisho wa msimu wa 2025/26.

Baada ya ada kuafikiwa kati ya klabu, kilichokatisha tamaa ya uhamisho wa kwenda Manchester United msimu wa majira ya joto wa 2022 baada ya kuwasili kwa Ten Hag ni ukosefu wa ufafanuzi juu ya nani atamlipa mchezaji huyo deni lake la mshahara uliosimamishwa na Barca.



# MAN CITY WAJITOSA KWA BRANTHWAITE

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City wanafuatilia maendeleo kuhusu mlinzi wa Everton, Jarrad Branthwaite, kwa mujibu wa ripoti.

Branthwaite amefurahia msimu mzuri pale Goodison Park licha ya vita vinavyoendelea vya 'The Toffees' hao dhidi ya kushushwa daraja kutoka Ligi Kuu England, na jana Jumanne alitarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza kwa kikosi cha England dhidi ya Ubelgiji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akihusishwa sana na kuondoka Everton katika miezi ya hivi karibuni kutokana na kiwango chake kizuri na hali mbaya ya kifedha ya klabu.

Ripoti ya Daily Mail imedai Man City ndiyo timu ya hivi karibuni zaidi kuweka wazi mpango wao kwa Branthwaite, ambaye amecheza mechi 35 pekee za Ligi Kuu England katika maisha yake ya soka.

Mabingwa hao watetezi wanasemekana kuvutiwa na umri wake, hali ya nyumbani na kufanana na John Stones, ambaye alihama kutoka Everton mwaka 2016.

Mbali na City, Mail inaongeza kuwa Manchester United, Real Madrid na Tottenham Hotspur pia wanavutiwa na Branthwaite.

90min ilifichua mapema mwezi huu kwamba United na Madrid wanavutiwa na Branthwaite, lakini wanaweza kushidwa na bei ya Everton ya pauni milioni 70.

United bado haijatayarisha orodha ya wachezaji wanaolengwa kwenye dirisha la majira ya joto huku INEOS na Sir Jim Ratcliffe wakiendelea na kazi ya kurekebisha nyuma ya pazia, ingawa Michael Olise wa Crystal Palace ni jina linalopendwa.

# *Bayern yampa tarehe ya mwisho Davies*

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imemuonya beki wake wa kushoto, Alphonso Davies, kwamba ana hadi mwisho wa mwezi kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo, ripoti imedai.

Davies ameingia miezi 18 ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na Bayern wanatarajia kumuongezea mkataba, lakini Mkurugenzi wa Michezo, Max Eberl, hivi karibuni alikiri klabu hiyo haiwezi kusubiri jibu milele.

Kinachotatiza mambo kwa Bayern ni dhamira ya Real Madrid kumsajili Davies msimu unaokuja wa majira ya joto.

Timu hiyo ya Hispania inatumai Davies atakataa ofa ya mkataba mpya, ambao utailazimu Bayern kumuuza kwa ada iliyopunguzwa.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Bayern wanataka jibu kutoka kwa Davies ifikapo mwisho wa mwezi huu. Iwapo ataamua kukataa kuongezewa muda, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Canada atapatikana kwa uhamisho na Bayern wanataka muda wa kutosha kutafuta nyongeza ya kiwango cha juu.

Wachezaji wengine kama Theo Hernandez wa AC Milan na Ian Maatsen wa Chelsea wametajwa kuwa wanaweza kuchukua nafasi ya Davies.

Davies anaripotiwa kudai mkataba mpya wenye thamani ya euro milioni 20 kwa mwaka, lakini ofa ya Bayern ina thamani ya euro milioni 14 kwa msimu.

Ikiwa Bayern watalazimika kuachana na Davies msimu huu wa majira ya joto, watadai ada ya angalau euro milioni 50, lakini Madrid wanafanya kazi "kwa nguvu zao zote" kupunguza kiasi hicho.



# Vinicius: Nahisi kukosa hamu ya kucheza

**MADRID,** Hispania

WINGA wa Brazil, Vinicius Jr amesema anahisi kama hana hamu ya kucheza soka kwa sababu ya unyanyasaji wa mara kwa mara wa kibaguzi aliofanyiwa.

Msimu uliopita kulikuwa na matukio 10 ya aina hiyo dhidi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, yaliyoripotiwa kwa waendesha mashtaka na LaLiga.

Wakati wa mkutano wa waandishi wa habari jana, Vinicius alisema kuwa hataondoka Real Madrid na Hispania, kwani kwa kufanya hivyo ataruhusu ubaguzi wa rangi kushinda.

Hata hivyo, alisema alikuwa anaona ni "vigumu kusonga mbele" kutokana na unyanyasaji huo.

Brazil jana ilicheza na Hispania katika mechi ya kirafiki ya kimataifa kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu mjini Madrid kama sehemu ya kampeni ya kupinga ubaguzi wa rangi chini ya kaulimbiu 'Ngozi Moja'.

Vinicius alisema: "Hakuniingia akilini kuondoka Hispania kwa sababu nikiondoka nitawapa wabaguzi kile wanachotaka.

"Nitabaki kwa sababu kwa njia hiyo wabaguzi wa rangi wanaweza kuendelea kuniona usoni zaidi na zaidi.

"Mimi ni mchezaji shupavu, nacheza Real Madrid na tunashinda mataji mengi na hilo haliwafurahishi watu wengi.

"Nataka tu kucheza soka, lakini ni vigumu kusonga mbele; najihisi kutopenda kucheza."



HABARI MICHEZO

# Morocco: Bado nina kazi ya kufanya Stars

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Timu ya Taifa ya Mongolia juzi, mechi iliyochezwa Uwanja wa Dalga Arena nchini Azerbaijan, Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Suleiman 'Marocco', amesema bado ana kazi ya kufanya kuinoa safu ya ushambuliaji kwani katika mchezo huo imeonekana kukosa mabao mengi ya wazi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya mashindano maalum ya FIFA Series 2024 iliyopigwa juzi, Morocco alisema nafasi nyingi zilizokuwa zinapatikana na kupotezwa, wakati mwingine hupatikana chache katika michezo mingine ya mashindano makubwa, hivyo inabidi zitumiwe vema.

"Kwa mimi, lakini bado nina kazi ya kufanya, kwa sababu tumetengeneza nafasi nyingi, tulikuwa tufunge mabao zaidi ya hayo, katika baadhi ya mechi za mashindano makubwa nafasi zile unazipoteza inakuwa shida, lakini pia huwezi kupata nafasi nyingi kama zile, utapata chache na unatakiwa kuzitumia, nafikiri tunapanda kidogo kidogo, lakini pia tuna kazi ya kufanya," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya mashindano hiyo, atakuwa na kazi ya kurekebisha hali hiyo katika michezo inayofuata huko mbele.

Akiizungumzia mechi hiyo, kocha huyo alisema kipindi cha kwanza hali ilikuwa ngumu kwa sababu wapinzani wao walipaki basi, lakini kipindi cha pili walibadilisha mfumo na kuweza kupata idadi hiyo ya mabao ambayo kwake anasema yalikuwa ni machache kuliko nafasi zilizopatikana.

## P Diddy atoweka, Usalama wamsaka

INATOKA UKURASA 24

pia ilikuwapo katika kusaidia zoezi hilo.

Wanawake ambao wametoa shutuma hadharani dhidi ya Diddy wameonesha kufurahishwa na uvamizi huo wa nyumba za P Diddy.

Wakili Douglas Wigdor, anayemwakilisha Cassie Ventura na mlalamikaji ambaye jina lake lilijulikana kama Jane Doe, alitoa taarifa hii:

"Siku zote tutaunga mkono utekelezaji wa sheria unapotaka kuwafungulia mashtaka wale ambao wamekiuka sheria. Tunatumaini huu ni mwanzo wa mchakato ambao utamshikilia P Diddy kuwajibika kwa mwenendo wake potovu."

Majumba mawili yalifanyiwa uchunguzi huko Los Angeles na Miami kama sehemu ya uchunguzi.

Hata hivyo, wawakilishi wa rapa huyo hawakuwa tayari kuzungumzia zoezi hilo.

Pia, P Diddy mwenyewe imedaiwa kwamba aliondoka mapema kwa ndege binafsi kuelekea kusikojulikana.

Mwaka jana, mwimbaji wa R&B, Cassie, ambaye jina lake kamili ni Casandra Ventura, aliwasilisha kesi katika mahakama ya shirikisho ya New York dhidi ya Combs, ambaye walikuwa wamechumbiana kati ya 2005 na 2018.

Wanawake wengine wawili wakajitokeza na kesi zao, wakimtuhumu kwa unyanyasaji wa kijinsia.

# KIBADENI AMTAKA AYOUB LANGONI SIMBA VS AL AHLY

**Na Saada Akida**

MCHEZAJI wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na Klabu ya Simba, Abdallah 'King' Kibadeni, ameliomba benchi la ufundi la timu yake hiyo kumpanga kipa Ayoub Lakred katika mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Simba itaikaribisha Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Ijumaa wiki hii kabla ya kwenda kurudiana Aprili 5, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Cairo, Misri na mshindi wa jumla atatinga nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kibadeni alisema ameangalia baadhi ya mechi ambazo makipa wote walicheza na kuona Manula ameshuka kiwango kidogo kutokana na majeraha ambayo aliyapata huko nyuma, Ayoub raia wa Morocco akiwa kwenye kiwango cha juu kwa sasa.

**Alisema, licha ya Kaseja kupona na kurejea uwanjani, lakini anaamini hajawa fiti jambo ambalo lilimfanya kuruhusu mabao matano katika mechi dhidi ya Yanga.**

"Tutampa lawama sana Manula, hivi karibuni hayupo katika ubora alikuwa nao awali, kwa sababu ametoka katika majeraha makubwa na anatakiwa kupewa mechi zisizo na ushindani mkubwa kwa sasa yule kipa kutoka Morocco (Ayoub) yupo vizuri apewe nafasi ya kucheza ikiwezekana hii mechi ya Ijumaa dhidi ya Al Ahly.

Alisema anaimani kubwa kwa Simba kufanya vizuri dhidi ya Al Ahly, sina mashaka na benchi la ufundi, wana kocha Benchikha (Abdelhak), mzuri anauzoefu na hii michuano, kikubwa wachezaji wanatakiwa kuelewa kuwa wamebeba mioyo ya watu wengi," alisema Kibadeni.

Aliongeza kuwa viongozi wanatakiwa kukaa na wachezaji kuzungumza nao kuhusu umuhimu wa mchezo huo dhidi ya Al Ahly ili kupambana na kuwapa burudani mashabiki na wanachama ambao wanaumia pale Simba inapofanya vibaya.

"Binafsi nimekuwa na wakati mgumu sana juu ya Simba inapofanya vibaya, ninaimani katika mchezo wa Ijumaa tutafanya vizuri, kikubwa Wanasimba tushirikiane na kuwa wamoja tukifanya hivyo tunaweza kumuondoa Al Ahly kama ilivyo miaka ya nyumba, alivyoondolewa Zamalek ya Misri," alisema Kibadeni.

Kuhusu viwango vya wachezaji wawili, Freddy Michael na Pa Omar Jobe, waliosajiliwa dirisha dogo, alisema kama kocha hana mashaka na wachezaji hao na wanatakiwa kupewa muda.

"Ni mapema sana kuwazungumzia hao wachezaji hawana muda mrefu ndani ya timu, katika usajili hasa nyota wa kigeni kuna mambo mengi sana, kwanza ni mazingira ya kuyazoea, lakini na aina ya wenzake aliokutana nao katika timu husika, mfano ukimchukuwa Lionel Messi akija hapa atakuwa na ubora huo?," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba anayeshikilia rekodi ya kufunga 'hat-trick' kwenye dabi dhidi ya Yanga.



Wachezaji wa Simba wakirejea jijini Dar es Salaam wakitokea kambini Zanzibar, tayari kwa mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri, itakayopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

## Pigo Al Ahly, Mamelodi

INATOKA UKURASA 24

African Football League (AFL), na kutuondoa kikanuni, pasi na shaka kila mmoja wetu tunajua hilo, lakini tunahitaji kutumia uwanja wa nyumbani kutafuta ushindi mnono ambao tutawatoa wapinzani hapa nyumbani," alisema Kajula.

Kwa upande wa Yanga, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema jana kuwa, baada ya kujichimbia kambini kwa muda, kocha Gamondi amewahakikishia kuwa kikosi hicho tayari kimeiva kwa ajili ya mchezo huo wa robo fainali, hivyo kuwa na uhakika wa kufanya vema katika mechi ya kwanza itakayochezwa Jumamosi Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa habari huyo alisema wana imani ya kupata ushindi katika mchezo wa kwanza kwa sababu wapinzani wao pia wana baadhi ya wachezaji ambao hawatocheza kwa kuwa majeruhi na adhabu kikanuni.

"Niwaibie tu siri Wanayanga kuwa hata Mamelodi pia wana wachezaji wao ambao ni majeruhi na wengine ambao hawatocheza mechi hiyo kutokana na kuwa na kadi tatu za njano, kwa hiyo wasiwe na wasiwasi, tutatumia udhaifu huo kuwashangaza," alisema Kamwe.

# Michezo

Jumatano Machi 27, 2024

Nipashe




De Jong haondoki Barca - Laporta UKURASA 21



Emam Ashour - Al Ahly




Kocha Rulani Mokwena wa Mamelodi na mchezaji wake, Themba Zwane, atakayeikosa mechi ya Yanga

## P Diddy atoweka, Usalama wamsaka

**LOS ANGELES,** Marekani

MAWAKALA wa Usalama wa Marekani jana walivamia jumba la rapa, Sean "Diddy" Combs au Puff Daddy lililoko Holmby Hills kwa ajili ya uchunguzi, huku yeye mwenyewe akitokomea kusikojulikana.

Sababu hasa ya uvamizi huo bado haijawekwa wazi, lakini P Diddy hivi karibuni amehusishwa na madai ya unyanyasaji wa kijinsia na biashara ya ngono.

Mawakala hao walivamia jumba hilo katika mtaa wa 200 wa S. Mapleton Drive huko Holmby Hills, eneo la matajiri la Los Angeles linalojulikana kama mitaa ya watu mashuhuri na jumba la Playboy.

Jumba hilo linahusishwa na Kampuni ya Utengenezaji wa Filamu za Bad Boy ya Combs.

Mawakala hao walionekana wakiwashikilia wanaume wawili ambao baadaye walitambuliwa kuwa ni watoto wa Diddy, na kwamba vijana hao walizuiliwa nje huku upekuzi ukiendelea ndani ya jumba hilo.

"Mapema leo (jana), uchunguzi wa Usalama wa nchi (HSI) New York, ulichukua hatua za kutekeleza sheria kama sehemu ya uchunguzi unaoendelea, kwa usaidizi kutoka kwa HSI Los Angeles, HSI Miami, na washirika wetu wa kutekeleza sheria katika eneo husika.

"Tutatoa taarifa zaidi kadri zitakavyopatikana," ilisema taarifa ya Idara hiyo ya Usalama wa nchi katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari.

Idara ya kipolisi ya Sheriff ya Los Angeles

INAENDELEA UKURASA 23

# PIGO AL AHLY, MAMELODI, KICHEKO SIMBA, YANGA

**Adam Fungamwango na**

**Saada Akida**

●●● Majeruhi yaandama vikosi vyao vya kwanza wakati zikitua nchini leo kwa...

WAKATI wapinzani wa Simba na Yanga kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly na Mamelodi wakitarajiwa kutua nchini leo tayari kwa mechi zitakazopigwa Ijumaa na Jumamosi, taarifa zimeeleza kuwa vikosi vyao vinakabiliwa na wimbi kubwa la majeruhi.

**Simba itaikaribisha Al Ahly ya Misri katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Ijumaa wiki hii kabla ya kesho yake, Jumamosi Yanga kuwa mwenyeji wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini uwanjani hapo.**

Kuelekea mechi hizo kwa mujibu wa vyombo mbalimbali vya habari Misri na Afrika Kusini, wachezaji majeruhi kwa upande wa Al Ahly ni kiungo mshambuliaji Allou Dieng anayeuguza goti, golikipa Mohamed El Shenawy, mwenye majeraha ya bega, na kiungo mkabaji Emam Ashour aliyeumia bega wote wakiwa ni wa kikosi cha kwanza.

Kwa upande wa Mamelodi Sundowns, imeripotiwa kuwa kiungo mshambulaji Muargentina Junior Leandro Mendieta, golikipa tegemeo, Ronwen Williams, Thapelo Maseko ni majeruhi pamoja na Teboho Mokoena, huku kiungo mshambuliaji Themba Zwane akiukosa mchezo huo kutokana na kadi tatu za njano, lakini pia imeelezwa naye ni majeruhu.

Hata hivyo, habari nzuri kwa Mamelodi ni kwamba wachezaji wengine majeruhi wamepata nafuu, nao ni Mothobi Mvama na Khuliso Mudau.

Uongozi wa Simba umesema umeandaa silaha mbili zitakazoisaidia timu yao kufikia malengo yao ya kufanya vizuri na kutinga nusu fainali msimu huu.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, jana aliweka kuwa wazi silaha hizo kuwa ni kutilia maanani matakwa ya benchi la ufundi linaloongozwa na Abdelhak Benchikha pamoja na wachezaji, lakini na mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani.

Kajula alisema kwa misimu kadhaa Simba imekuwa ikiishia hatua ya robo fainali, lakini wamefanya majaribio ya makusudi na mahususi kwa safari hii kwenda nusu fainali.

Alisema majaribo hayo ni kuandaa silaha hizo ikiwamo kumsikiliza Benchikha mahitaji yake kwa kupata mazingira mazuri ya kambi kwa timu kujichimbia visiwani Zanzibar kwa ajili maandalizi ya mchezo huo na silaha nyingine ni mashabiki ambao wamekuwa wakiisapoti timu wakati wote.

"Timu ilipokuwa Zanzibar tulipata mechi ya kirafiki ambayo imetupa maandalizi mazuri sana, kocha imempa ufundi, kuona madhaifu ya kikosi chake pamoja na wale waliopo Taifa Stars kurejea na kuungana na wenzao, Chama (Clatous) na wengine watarudi muda wowote kuanzia leo na kuungana na timu kambini.

"Tunaiheshimu Al Ahly ni timu bora, lakini tukumbuke tumekutana nao katika robo fainali ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >